# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## 2020 - 2025

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. Masoud Ali Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |
| 9. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. | Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge.** |
| **11. Mhe.** | **Dkt. Soud Nahoda Hassan** | **-** | **MBM/Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje** |
| **12. Mhe.** | **Simai Mohammed Said** | **-** | **MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu** |
| **13. Mhe.** | **Tabia Maulid Mwita** | **-** | **MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais** |
| **14. Mhe.** | **Riziki Pembe Juma** | **-** | **MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake** |
| **15. Mhe.** | **Rahma Kassim Ali** | **-** | **MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake** |
| **16. Mhe.** | **Suleiman Masoud Makame** | **-** | **MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga** |
| **17. Mhe.** | **Abdulla Hussein Kombo** | **-** | **MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani** |
| **18. Mhe.** | **Lela Muhamed Mussa** | **-** | **MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake** |
| **19. Mhe.** | **Abdalla Abasi Wadi** | **-** | **Jimbo la Nungwi** |
| **20. Mhe.** | **Ali Abdulgulam Hussein** | **-** | **Jimbo la Jang’ombe** |
| **21. Mhe.** | **Ali Suleiman Ameir** | **-** | **Jimbo la Pangawe** |
| **22. Mhe.** | **Ameir Abdalla Ameir** | **-** | **Jimbo la Mwanakwerekwe** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |
| 29. Mhe. | Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 30. Mhe. | Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 31. Mhe. | Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |
| 32. Mhe. | Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 33. Mhe. | Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 34. Mhe. | Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 35. Mhe. | Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 36. Mhe. | Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 37. Mhe. | Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. | Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 39. Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 40. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 41. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 42. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 43. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 44. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 45. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 46. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 47. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 48. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 49. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |
| 50. Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 51. Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 57. Mhe. | Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. Mhe. | Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. Mhe. | Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 63. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 64. 5Mhe. | Sabiha Filfil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 65. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 66. Mhe. | Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 67. Mhe. | Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 68. Mhe. | Suleiman Haroub Suleiman | - | Jimbo la Kiembe Samaki |
| 69. Mhe. | Sulubu Kidongo Amour | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 70. Mhe. | Shadya Mohamed Suleiman | - | Nafasi za Wanawake |
| 71. Mhe. | Shamata Shaame Khamis | - | Jimbo la Micheweni |
| 72. Mhe. | Shaib Hassan Kaduara | - | Jimbo la Chake Chake |
| 73. Mhe. | Yahya Rashid Abdulla | - | Jimbo la Kwahani |
| 74. Mhe. | Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 75. Mhe. | Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 76. Mhe. | Zawadi Amour Nassor | - | Jimbo la Konde |

| | | |
|---|---|---|
| Ndg. Raya Issa Msellem | - | Katibu |

**Kikao cha Sita - Tarehe 17 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

**TAARIFA YA MHE. SPIKA**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 10 Februari, 2021 Mhe. Shadya Mohammed Suleiman aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 15. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi.

Aidha, katika kikao cha tarehe 11 Februari, 2021 Mhe. Mihayo Juma N'hunga wa Jimbo la Mwera aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 54. Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi.

Sasa nawaomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi wasome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na wajumbe hao. Ahsanteni.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma:** Mhe. Naibu Spika, naomba kwa heshima kwanza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na Mawaziri wanaofuata waendelee wakati tukimsubiri Waziri wa Fedha ambaye amepata dharura kidogo anakuja.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri umeshajibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma:** Mhe. Naibu Spika, liliomba kwamba kutokana na dharura alilokuwa nazo Waziri wa Fedha ambaye atafika muda wowote sasa hivi naomba Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na Mawaziri wengine waendelee kwanza kutoa taarifa zao.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu kama suala ambavyo liliulizwa swali la nyongeza la Mhe. Mihayo Juma N'hunga, ambaye alitaka kujua je, kuna eka ngapi za akiba ili wananchi waweze kuziomba kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo.

Mhe. Naibu Spika, eka tatu ni jina la ardhi ya kilimo iliyotaifishwa baada ya Mapinduzi ya 1964 na kugaiwa na serikali kwa wananchi wanyonge waliokuwa hawana fursa au uwezo wa kupata ardhi kwa ajili ya kujikimu mahitaji yao ya kimaisha katika kipindi cha baina ya 1965 hadi 1974. Ardhi hizo za eka tatu ziligaiwa kifamilia chini ya *decree* Nam. 5 ya mwaka 1966 na marekebisho yake ya 10 ya mwaka 1967, ya 10 ya mwaka 1968, marekebisho nambari 1 ya mwaka 1969 na marekebisho nambari 3 ya mwaka 1982.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa jumla ya eka 13,364 ziligaiwa Unguja na eka 8,898 ziligaiwa huko Pemba. Hesabu hii ni sawa na ekari 66,786 za ardhi zilizogaiwa chini ya mfumo wa eka tatu. Eneo la ardhi ya eka tatu ni sawa na asilimia 28 kwa Unguja na asilimia 9 kwa Pemba ya eneo lote la kilimo.

Kutokana na maeneo mbali mbali  kubadilisha matumizi kutokana na utekelezaji wa Mpango Mkuu (*Master Plan*) ya mwaka 1982 ikwemo maeneo ya Kiembesamaki, Mombasa, Mpendae, Kaburikikombe, Mwanakwerekwe, Magogoni, Mtoni Kidatu. Hali hiyo ilichangia kupungua idadi ya eka zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Aidha, kutokana na tathmini zilizofanya kati ya mwaka 2010 hadi 2019 kwa upande wa Unguja, katika maeneo ya mbali mbali yakiwemo Shehia za Fuoni Kibondeni, Mwera Mtofaani na Mwera. Kati ya mashamba 260 ya Fuoni Kibondeni, 43 yameshaathiriwa na ujenzi. Mashamba ya eka tatu 606 yalikaguliwa katika upande wa Mwera.  Kwa upande wa Mwera Mtofaani kati ya mashamba 6,627 yamebadilishwa matumizi yake ikiwemo uchimbaji wa mchanga na ujenzi wa nyumba za makaazi.

Mhe. Naibu Spika, katika Shehia ya Kiembesamaki eka zote zimeshajengwa asilimia 29 ya eka za Chuini, 18 Kihinani na 4 Bububu ndiyo zinatumika kwa kilimo ambazo wanaozitumia bado wapo.

Wakati wa tathmini hiyo Shehia za Wilaya ya Kati na Kaskazini zilionekana zipo salama kidogo ukilinganisha na Shehia za Wilaya ya Magharibi.  Hata hivyo, hivi karibuni limejitokeza wimbi kubwa la ukataji wa miti na ubadilishaji wa ardhi ya eka tatu hasa mpakani mwa Wilaya hiyo na Wilaya za Magharibi ‘A’ na ‘B’.  Aidha, Shehia za Wilaya za Magharibi ‘A’ na ‘B’ ambazo zipo karibu na mji zimeathirika zaidi kuliko zile zilizopo mbali na mji.

Kutokana na hali hiyo ni dhahiri kwa sasa hakuna akiba ya eka tatu ambazo wananchi wanaweza kuziomba kama ni akiba ya eka badala yake ule utaratibu wa kuziomba baada ya watumiaji wa mwanzo kufariki unaendelea. Inasisitizwa wananchi kufuata utaratibu katika kuziomba eka hizo ili kuepusha migogoro kwa familia ambazo wanazitumia eka hizo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kunipa nafsi ya kujibu swali la nyongeza ambalo lilitokana na swali la msingi Nam. 15 Mhe. Shadya Mohammed Suleiman lilikuwa linahusu swali la kodi na naomba nijibu kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, jumla ya kodi Tzs 379,569,349.84 zilikusanywa kutokana na mauzo ya Tzs. 3,073,481, 227 na kuingia serikali katika muda wa majaribio ambao wafanyabiashara hao wameanza kutumia mfumo huu wa kielectroniki. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 56**

**Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**Mhe. Habib Ali Mohamed** - Aliuliza:

Kuna kitengo kinajuilikana kama Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (*ZAECA*).

(a) Je, mamlaka ina umuhimu na faida gani nchini

(b) Je, kwa nini mamlaka hiyo inashindwa kuhoji suala la ununuzi wa meli ya MV. Mapinduzi II na uhalisia wake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi vinadhibitiwa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (*ZAECA*) kupitia Sheria Nam. 1 ya Mwaka 2012, Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar. Aidha, serikali imeendelea kuchukua hatua za udhibiti na uchunguzi wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar na kwa kipindi kirefu hivi sasa, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imekuwa ikipokea na kushughulikia kwa mujibu wa sheria tuhuma za makosa ya rushwa na uhujumu uchumi ili kuhakikisha kwamba masuala ya rushwa na uhujumu uchumi yanadhibitiwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tayari Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imekamilisha ripoti ya jitihada za kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar kwa mwaka 2020. Ripoti hiyo inasuburi kujadiliwa katika mkutano wa Baraza lako la Wawakilishi unaoendelea hivi sasa ambao tayari waheshimiwa wameshakabidhiwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ina umuhimu mkubwa sana katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar kutokana na kazi zake za kila siku kama zilivyoainishwa katika kifungu cha 13 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nam. 1/2012. Miongoni mwa kazi hizo zenye umuhimu mkubwa katika jamii ni kama hizi zifuatazo:-

- Kushauri taasisi za serikali juu ya namna bora ya kuepukana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi hapa Zanzibar.

- Kuelimisha wananchi juu ya hatari ya rushwa na uhujumi uchumi na namna gani rushwa inavyorudisha nyuma maendeleo endelevu ya Zanzibar.
- Kurudisha mali/fedha za serikali ambazo zimechukuliwa kinyume na utaatibu.
- Kuchunguza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.
- Kusaidia taasisi yoyote ya serikali inayosimamia sheria katika kufanya uchunguzi wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

(b) Kama nilivyotangulia kueleza katika maelezo yangu ya msingi Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imeendelea kushughulikia na kuchukua hatua za udhibiti na uchunguzi wa makosa mbali mbali ya rushwa na uhujumu uchumi kwa mujibu wa sheria na taratibu za kiuchunguzi. Baada ya kupokea taarifa za tuhuma za makosa hayo zinazotolewa na wananchi au kupatikana kupitia vianzio mbali mbali vya mamlaka.

Kwa sasa Mamlaka inaendelea na uchunguzi wa taarifa ya ununuzi wa Meli ya MV. Mapinduzi II na hatua mbali mbali za kiuchunguzi tayari zimeshachukuliwa ikiwemo kuwahoji baadhi ya wahusika, kupitia nyaraka muhimu za ununuzi wa meli hiyo pamoja na kupatikana kwa wataalamu watakaosaidia uchunguzi wa Taasisi ya Ununuzi wa MV. Mapinduzi II.

Serikali kupitia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi mara tu baada ya kukamilisha kwa hatua hizo za uchunguzi wa ununuzi wa meli hiyo na endapo itabainika kuwepo kwa kasoro yoyote katika utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa meli hiyo na uhalisia wake zitachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na taratibu.

**Mhe. Habibu Ali Mohamed:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa unapomalizika msimu wa karafuu wakulima wengi huwa wanahifadhi karafuu zao ndani ya majumba yao, na hizi inasaidia kipindi kile ambacho wana shughuli za harusi, mazishi wanaweza wakachukua karafuu zile kidogo kidogo wakaziuza mpaka zikamalizika, kwa sababu kuna wakulima wengine hawana *account bank*, kwa hivyo, tegemeo lao ni kuweka karafuu majumbani msimu unapomalizika wanaweka kidogo kidogo wanauza. Hii imetokezea tokea miaka ya nyuma tokea sisi tupo wadogo kinaendelea mpaka sasa hivi.

Je, ni taaasisi gani au mamlaka gani inayopaswa kumkamata mtuhumiwa wakati wa usiku nyumbani kwake ni polisi, Idara Maalum ya Vikosi vya SMZ au *ZAECA*.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, naona ni swali jipya sasa kama nijibu tu nitajibu lakini swali la msingi ni umuhimu wa *ZAECA*, sasa naulizwa habari ya kukamata magendo ya karafuu...

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa uko sahihi sio swali la msingi kwa hiyo inawezekana sana ulijibu, lakini kwa manufaa labda ya wananchi au na yeye mwenyewe kama una majibu yake basi pia unaweza kumjibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Nijibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Ndio.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, kazi ya *ZAECA* baada ya kupata taarifa kwamba kuna mtu amehifadhi mali mahali kinyume na utaratibu wa kisheria basi wanaweza kwenda kufanya uchunguzi na wakibaini wanachukua hatua. Lakini kuna kikosi maalum ambacho kinashughulikia suala hilo, nadhani suala la kukamata magendo ni kazi ya KMKM na hao ndio wenye jukumu kubwa la kukamata pamoja na viongozi wa Shehia, Wilaya na Mikoa ndio wanaosimamia masuala katika maeneo yao.

**Mhe. Saada Mkuya Salum:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Naibu Spika, kuna utaratibu ambao unaendelea sasa hivi, kuna watu kwa mfano wanaokaa katika majumba ya Michenzani na inatokea wamechelewa kulipa labda kodi *or something like that.* Kinachotokea sasa hivi *ZAECA* wanatuma magari wanakwenda kuwachukua wale yaani sio *Zanzibar Housing Cooperation* (*ZHC*) ni *ZAECA* ndio wanatuma magari wanachukuliwa wale watu mara nyengine wengine wengi ni watu wazima wanapelekwa *ZAECA*, na huko *reception* ya *ZAECA* wanaoifahamu ni wao tu.

Sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri hivi ni utaratibu gani ambao *ZAECA* au ni mamlaka gani ambayo *ZAECA* inayo kwenda kuwachukua watu ambao pengine wana madeni na kwenda kuwapeleka pale kuwahoji *as if* ni wahalifu, wengine wanaweza kuwa wana madeni 200,000 au 300,000 lakini sasa chombo hiki kimekuwa kama ni chombo ambacho askari au chombo kingine. Sasa tunaomba tujue kama haya mamlaka inayo *ZAECA* na kwa utaratibu upi unafanyika jambo hili. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, *ZAECA* kwa mujibu wa Sheria Nam. 1 ya 2012 wana mamlaka ya kumuhoji mtu yeyote kisheria wa ngazi yoyote ile, hiyo ndio sheria ambayo inawapa mamlaka hiyo. Sasa kama wanatumia busara ndio vizuri zaidi, kama hawatumii busara ni suala la kuwaelekeza ili watumie busara katika kwenda kuchukua hatua hizo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na yaliyopangika. Katika majibu yake amesema kwamba Taasisi ya *ZAECA* kazi zake ni kuchunguza, kushauri, kuelimisha na kurudisha mali na fedha ambazo zimechukuliwa na kurejeshwa serikalini. Je, ni mali gani zilizochukuliwa na fedha zilizochukuliwa ambazo tayari zimesharejeshwa serikalini baada ya kukamilika uchunguzi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa wangefanya subira kidogo kuna taarifa kamili ambayo itawasilishwa hapa Barazani inaeleza maelezo yote au jawabu zote zitapatikana kuhusu maswali yake Mhe. Mwakilishi.

Hata hivyo, kwa vile unataka orodha kamili ya mali zilizopatikana, aina gani, fedha zilizokusanywa hesabu hizo zipo na ukizitaka nitakuletea kimaandishi tukijaaliwa.

**Nam. 46**

**Changamoto kwa Baadhi ya Taasisi za Serikali Kutumia Kampuni Binafsi za Ulinzi**

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa** - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Kampuni ya Wakala wa Ulinzi kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Hata hivyo, pamoja na kuanzishwa wakala huo, bado hadi sasa baadhi ya taasisi za serikali zinaendelea kutumia kampuni binafsi za ulinzi na kuisababishia serikali hasara kubwa.

(a) Kwa kuwa lengo la kuanzisha wakala huo ni kuondoa utitiri wa kampuni za ulinzi na kuipunguzia serikali mzigo wa gharama za ulinzi. Je, ni hatua gani serikali itachukua kukabiliana na tatizo hilo.

(b) Ni taasisi gani za serikali ambazo bado zinaendelea kutumia walinzi binafsi badala ya Wakala wa Serikali.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lenye vifungu (a) na (b). Kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, malengo ya kuanzishwa kwa Sheria Nam. 2 ya Mwaka 2015 Sheria ya Wakala wa Ulinzi JKU yanaelezwa chini ya kifungu cha 5(a)(b) na (c) cha sheria hiyo ambayo ni kusimamia na kuboresha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii kwa taasisi za umma na taasisi binafsi. Kusimamia na kuboresha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii kwa kutambua ni maeneo muhimu ya uchumi wa nchi na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za ulinzi zilizo bora na uhakika. Kwa mujibu wa sheria hii lengo halikuwa huduma za ulinzi kwenye Taasisi za Serikali kama wengi wanavyodhania, bali ilikuwa ni kuwahakikishia wawekezaji wanapata huduma bora za ulinzi katika maeneo yao ikiwemo maeneo ya utalii hasa ikizingatiwa mahitaji ya soko la ulinzi yamekuwa ni makubwa katika sekta ya uwekezaji, utalii na Taasisi za Serikali na binafsi.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, Wakala wa Ulinzi wa JKU unatumika kutoa huduma za ulinzi kwa sekta binafsi, sekta za umma na hata mtu binafsi. Aidha, wakala haikuanzishwa kuziondoa kampuni binafsi za ulinzi zinazotoa huduma katika maeneo kadhaa, isipokuwa kuwepo kwa wakala kunasaidia kuzisimamia kampuni hizo kuweza kutoa huduma za ulinzi kwa ubora na uhakika. Kwa mnasaba huo, serikali haijakataza taasisi zake kupata huduma za ulinzi kutoka kwa kampuni binafsi jambo la msingi ni kuzingatia sheria za manunuzi na maslahi ya umma

wakati wa kuajiri kampuni hizo. Aidha, zipo Taasisi za Serikali zinapatiwa huduma na Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) pamoja na Jeshi la Polisi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mahitaji ya soko la ulinzi ni makubwa kwa sasa, serikali ina mpango wa kujenga uwezo zaidi kwa Wakala wa Ulinzi JKU ili iweze kutoa huduma kwa Taasisi za Serikali, sekta binafsi na watu binafsi. Kwa hivi sasa, Wakala wa Ulinzi JKU unatoa huduma katika taasisi 104 wakati soko la utalii tu peke yake lina taasisi zisizopungua 250 na lengo letu kuu ni kukamata fursa iliyopo kwenye utalii na uwekezaji ambapo tutatanua fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu na kusaidia kuinua uchumi wa nchi yetu. Kwa mantiki hiyo, naomba nikiri kwamba tuna uhaba wa walinzi na vifaa vya kisasa vya ulinzi kuweza kumudu kutoa huduma za ulinzi kwenye Taasisi za Serikali na sekta binafsi. Hivyo basi, kwa kuelewa mapungufu tuliyonayo mipango yetu kwa sasa ni kujenga uwezo zaidi wa Wakala wa Ulinzi JKU.

(b) Mhe. Naibu Spika, zipo Taasisi nyingi za Serikali ambazo hazijafikiwa bado na huduma za ulinzi zinazotolewa na Wakala wa Ulinzi JKU. Hata hivyo, baadhi ya Taasisi za Serikali zinazopatiwa huduma za ulinzi na Wakala wa Ulinzi wa JKU ni hizi zifuatazo:-

1. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*)
2. Afisi ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*)
3. Taasisi ya Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Afisi ya Zanzibar)
4. Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (*ZIPA*)
5. Kamisheni ya Utumishi wa Umma
6. Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*)
7. Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (*ZAECA*)
8. Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*ZURA*)
9. Shirika la Maendeleo ya Petroli (*ZPDC*)
10. Mamlaka ya Mafuta na Gesi (*ZPRA*)
11. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
12. Mamlaka ya Maji (*ZAWA*)
13. Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) na
14. Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*).

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri, marefu ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Ni taasisi ngapi zinazotumia wakala wa ulinzi, Unguja ziko ngapi na Pemba ziko ngapi.
(b) Je, mapato yanayotokana na malipo ya huduma ya ulinzi unaofanywa na wakala wa ulinzi yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

(a) Taasisi nilizozitaja ni zile ambazo ndio zinapata huduma ya Wakala wa Ulinzi wa JKU, ambazo sikuzitaja zote Unguja na Pemba hazipati huduma hiyo.
(b) Mapato yanayokusanywa na wakala wa Ulinzi wa JKU, mapato haya yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri ametueleza kwamba fedha zinazokusanywa na Wakala wa Ulinzi wa JKU zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Tunamuomba Mhe. Waziri atwambie kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni kiasi gani cha fedha ambacho kimeingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Lakini pili ni kwamba fedha nyingi zinakusanywa kupitia Wakala wa Ulinzi na wamekiri kwamba kuna uhaba wa walinzi na vifaa vya kisasa. Je, ni mikakati gani ambayo wameipanga kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake la nyongeza lenye vipengele viwili kama ifuatavyo:

Ni kweli fedha hizi zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ila nimuahidi kumletea *figure* halisi yaani kiasi gani ambacho kimeingizwa katika mwaka huu wa fedha.

Jibu lake la pili ni kwamba vifaa kama nilivyotanguliza kusema katika jawabu langu la msingi ni kweli tuna upungufu wa vifaa katika kufanya ama kuleta ufanisi zaidi kwa Wakala wa Ulinzi wa JKU. Mpango tuliokuwanao ni kwa mwaka wa fedha huu tunaokwenda kuuanza 2021/2022 kuimarisha ama kutengeneza utaratibu maalumu wa kumpa wakala vifaa vya kutosha ili aweze kutoa huduma hii kiufanisi zaidi.

**Nam. 60**

**Ushirikishwaji wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali**

**Mhe. Habibu Ali Mohamed** - Aliuliza:

Wakati dunia inasisitiza juu ya suala la ujasiriamali, jumuiya zisizo za kiserikali na makundi mengine ya ushirika limekuwa ni suala ambalo limeitikiwa na wadau wengi, lakini suala hilo limekosa ustawi nchini kwa maslahi ya umma.

(a) Je, ni vipi jumuiya zisizo za kiserikali zitapewa uhuru wa kutekeleza majukumu na kazi zao bila ya kikwazo chochote.

(b) Je, wadau hawa muhimu wanashirikishwaje katika ujenzi wa nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Jumuiya Zisizo za Kiserikali baada ya kukamilisha taratibu za kisheria na kusajiliwa wanakuwa na uhuru kamili wa kutekeleza malengo yao ili mradi hawavunji sheria za nchi. Kazi kubwa inayofanywa na Afisi ya Mrajis wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali ni kusajili, kuratibu na kusimamia jumuiya hizo ili ziweze kutekeleza malengo yao ipasavyo kwa mujibu wa sheria na pia kuzihamasisha kuwasilisha ripoti zao za utendaji kazi pamoja na ripoti za fedha ili kufahamu mchango halisi unaotolewa na Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika maendeleo ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inathamini sana juhudi zinazofanywa na Jumuiya Zisizo za Kiserikali nchini jambo lililopelekea kukuza mashirikiano endelevu yanayowawezesha jumuiya kufanya kazi zao kwa uhuru na kuwajibika kuongeza ufanisi zaidi na kuleta tija kwa wananchi. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi amekutana na jumuiya mbali mbali na kufanya mazungumzo nao juu ya kujenga nchi yetu. Aidha, katika Tamasha la (14) la Jumuiya Zisizo za Kiserikali lilifunguliwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye alikuwa ni Mgeni Rasmi kwa niaba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hali hii inaonesha wazi kuwa Jumuiya Zisizo za Kiserikali nchini zinapewa uhuru na kuthaminiwa na pia wanapata mashirikiano makubwa ya serikali na viongozi wakuu wa nchi.

(b) Mhe. Spika, kwa kuzingatia kwamba Jumuiya Zisizo za Kiserikali ni wadau muhimu wa maendeleo ya nchi, serikali imeendelea kuwashirikisha katika kujenga nchi yetu na kuwapa ushauri elekezi juu ya kuimarisha utendaji wao wa kazi, kuanzisha miradi endelevu inayozingatia vipaumbele vya serikali na kuiunga mkono serikali katika kutatua changamoto mbali mbali zinazoikabili jamii. Hali hii, imepelekea Jumuiya Zisizo za Kiserikali kuongeza juhudi ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa kuanzisha miradi ya kujenga Vituo vya Afya, kusaidia huduma za afya na kutoa misaada ya vifaa tiba katika hospitali zetu. Vile vile, kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya maji na pia kusaidia watu wanaoishi katika mazingira magumu wakiwemo Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha *COVID-19* Jumuiya Zisizo za Kiserikali zilichukua juhudi za makusudi kuunga mkono serikali katika mapambano dhidi ya corona kwa kutoa elimu kwa wananchi kupitia redio na televisheni, kusambaza vipeperushi, kufanya mafunzo, semina na makongamano pamoja na kutoa vifaa mbali mbali vya kujikinga. Aidha, ziko jumuiya zinatoa elimu mbali mbali zikiwemo uhifadhi wa mazingira ya bahari unaopelekea uimarishaji wa Uchumi wa Buluu, elimu ya ujasiriamali na uanzishaji wa miradi ya kiuchumi. Juhudi hizi za Jumuiya Zisizo za Kiserikali zinazoendelea kufanyika ni matunda yanayotokana na ushirikishwaji mzuri unaofanywa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika ujenzi wa nchi yetu na kuwaletea maendeleo wananchi wote.

**Mhe. Habibu Ali Mohamed:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, napenda nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa huko nyuma tulikotoka kulikuwa na utitiri wa jumuiya ambazo nyengine zilikuwa haziko kisheria, nyengine ziko kisheria, namuuliza Mhe. Waziri je, baada ya zoezi hilo kukamilika ni jumuiya ngapi kisiwa cha Pemba ambazo zimesajiliwa kisheria na kisiwa cha Unguja ziko ngapi. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Jumuiya zote zilizosajiliwa Unguja na Pemba ni 2,403, kati ya hizo jumuiya zilizosajiliwa Unguja ni 2,214 na Pemba ni 189.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kipengele (a) na (b). Kwa kuwa Zanzibar imekumbwa na utitiri wa jumuiya hizi zisizo za kiserikali na kwa kuwa baadhi ya jumuiya hizi hazifanyi shughuli kwa mujibu wa sheria za kuanzishwa kwao.

(a) Je, serikali inalifahamu hili.
(b) Je, serikali ina mpango gani kwenye jumuiya hizi. Nakushukuru sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

(a) Ni kweli serikali inafahamu kwamba zipo jumuiya zisizo za kiserikali ambazo hazifuati taratibu na ziko nyingi, lakini kwa mujibu wa Sheria Nam.6 ya Uanzishwaji wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali ya Mwaka 1995 tunachukua ama tunafanya utaratibu wa uhakiki. Kwanza kufahamu shughuli anazozifanya, lakini pia kwa mujibu wa sheria ile kila jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake na matumizi ya fedha wanavyotumia, na ikionekana kwamba jumuia hizo hazifuati taratibu kwa mujibu wa sheria ile hatua tunazozichukua ni kuzifuta jumuiya hizo.

(b) Nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba zoezi hilo tumelianza na katika mwaka huu tumeanza kufanya uhakiki huo na mpaka Machi, 2021 tutakuwa tumekamilisha uhakiki wa jumuiya hizo kwa Unguja na Pemba.

**Nam. 79**

**Kiwanda cha Kuzalisha Maji cha Drop Kutowatendea Haki Watendaji Wake**

**Mhe. Bakar Hamad Bakar** - Aliuliza:

Kiwanda cha Kuzalisha Maji cha Drop kilichopo Wilaya ya Kati – Unguja kinalalamikiwa kuwafanyisha kazi watendaji wake hususan wanaozalisha maji kinyume na matakwa ya Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa.

(a) Je, serikali ina utaratibu gani wa kuvifuatilia viwanda vilivyopo kwa lengo la kuhakikisha kuwa vinatekeleza shughuli zake kama Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa.

(b) Je, serikali inatuahidi nini katika kuhakikisha kuwa haki za watendaji wa kiwanda hiki zinapatikana kama Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa inavyoelekeza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Kamisheni ya Kazi ambayo ipo chini ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina utaratibu maalum wa kufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi ndani ya taasisi binafsi kwa kila baada ya muda. Lengo hasa la ukaguzi huo ni kuhakikisha kwamba Sheria, Kanuni, na Mikataba ya Kimataifa inatekelezwa kwenye taasisi hizo kama inavyotakiwa.

(b) Kwa mujibu wa kaguzi zilizofanywa hapo awali na hata hivi karibuni kulionekana kwa namna fulani muajiri anatekeleza Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa kama inavyoelekeza. Hata hivyo, ukaguzi uliweza kugundua ukiukwaji wa Sheria ya Ajira katika suala zima linalogusa haki na stahiki za wafanyakazi, ambapo kasoro iliyojitokeza ni kukuta wafanyakazi hawapewi malipo ya ziada kwa saa za usiku *(night shift allowance)* ambayo ni 5% ya mshahara wao. Tayari muajiri ametakiwa kuhakikisha amelipa stahiki hiyo haraka iwezekanvyo. Aidha, Kamisheni ya Kazi kupitia wizara itaendelea kuifuatilia kwa karibu zaidi kuona kwa namna gani inatekeleza agizo hilo na pia kuona hakuna tena haki zinazokiukwa kwa wafanyakazi katika kiwanda hicho.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na majibu haya mazuri nina swali moja la nyongeza lenye kipengele (a) na (b). Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa sheria katika kiwanda hicho na kwa kuwa tayari wizara yake imeshaelekeza muajiri kulipa malipo hayo.

(a) Je, malipo hayo yataanzia madeni yale ya nyuma au madeni ya sasa.
(b) Ni kiasi gani wafanyakazi hao wanadai. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

(a) Kuhusu suala la ulipaji wa madeni mimi mwenyewe binafsi nilifanya ziada katika kiwanda hicho hivi juzi kwenda kulihakiki hili jambo na kupata undani wake, na tulikutana na *management* wamesema kwamba wafanyakazi ambao wanadai hawazidi 10, kwa sababu ni *night shift allowance* kwa hivyo wanaoingia ni watu wachache sana. Lakini wataangalia madeni yote tangu ambapo wameanza ku-*register* hili tatizo mpaka hapa tulipofikia. Hiyo ndio ahadi ambayo wametupa.

(b) Kuhusu *figures* naomba nitaleta hayo kwa maandishi.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b). Mheshimiwa moja kati ya haki za wafanyakazi wa taasisi binafsi ni mikataba na tumeshuhudia mara nyingi wafanyakazi hawa wakilalamika kuhusiana na suala hili.

(a) Je, wizara yake imejipangaje katika Awamu hii ya Nane ya kulimaliza suala hili.
(b) Anawaambia nini wafanyakazi hao wa taasisi binafsi kuhusiana na suala zima la kufukuzwa ovyo makazini. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe maswali yake kama ifuatavyo.

(a) Kuhusu suala la mikataba juzi tulipokwenda kufanya hiyo ziara tuliitisha mikataba na mimi mwenyewe pia niliihakiki, jambo kubwa ambalo tumegundua ni kwamba mikataba ile lugha ambayo inatumika wakati mwengine inakuwa ni ngumu sana kwa mfanyakazi kuelewa. Kwa hivyo, jambo la kwanza tumewaambia kwamba lazima wahakikishe kuwa lugha ambayo inatumika iwe ni Kiswahili, lakini muajiriwa kabla hajasaini ule mkataba ajue zile *terms* na *condition* zote ambazo zipo pale. Kwa hivyo, suala la mikataba ni suala ambalo kwanza tunalipa uzito mkubwa sana kuhakikisha kwamba mikataba yenyewe kwanza inakuwepo *on site.* Kwa sababu wakati mwengine unaweza ukakuta kwamba kuna mashirika mikataba mtu analala nayo nyumbani badala ya kuwepo kwenye *site*, na hilo tumewasisitiza kwamba lazima mikataba iwepo kwenye *site* maafisa kazi wetu wanapokuja waikague na wahakikishe kwamba wafanyakazi kabla hawajasaini basi wanaelewa nini ambacho wanakisaini. Tunatilia mkazo mkubwa katika jambo hilo.

(b) Kuhusu suala la kufukuzwa kazi watu kiholela. Hili tumeshalifanyia kazi tumeshalitolea msisitizo mkubwa sana. Hata hivi juzi nafikiri kama wiki tatu zilizopita tuliitisha *press conference* na kutoa waraka wa kutoa msisitizo kwa waajiri kwamba wazingatie sheria za nchi kuhakikisha kwamba watu wanapewa mikataba na wale ambao wako katika mikataba ya muda mfupi kuhakikisha kwamba wanatoa *notice* mapema endapo wanadhamiria kutoku-*renew* ile mikataba yao.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya serikali lakini na mimi naomba nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe Waziri atakubaliana na mimi kwamba moja kati ya changamoto inayoikabili Kamisheni ya Kazi ni uwepo wa kitengo finyu cha kufanya ukaguzi kuhusiana na mikataba ya ajira ya wafanyakazi wetu. Suala ambalo linapelekea baadhi ya kampuni kuchukua takribani miaka mitatu bila ya kutembelewa wala kukaguliwa, swali langu.

(a) Je, ni lini serikali sasa katika kuwasaidia wananchi wanyonge wa Zanzibar itaongeza nguvu katika kitengo hichi ili ukaguzi uwe unafanyika kwa wakati na usahihi kama inavyotakiwa.

(b) Je, serikali kupitia wizara yake iko tayari sasa pamoja na jitihada nzuri zinazoendelea kufanywa kupokea orodha ya kampuni ambazo hadi leo tunazungumza bado hazitoi mikataba kwa wafanyakazi na bado zinaendelea kuwanyonya kwa kutokuwalipa stahiki wafanyakazi hao. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Mhe Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Shaaban Ali Othman Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kama ifuatavyo:-

Kwanza, nikubaliane na yeye kwamba kitengo chetu cha Maafisa kazi kweli kiko finyu kina uhaba mchache sana wa Maafisa hao ambao kwa kweli unapowaingiza katika *rotation* kwenye *coverage* yao pengine inaweza ikawa *less than twelve percent.* Kwa hiyo, ni kweli *coverage* ni ndogo sana lakini hivi karibuni tume-*re-asign* Maafisa kazi wapya 12 kwa ajili ya kuongezea kwenye hiyo *pull* ili tuweze kupata *coverage* kubwa zaidi, hiyo bado haitoshi kuna haja kubwa ya kuendelea kuwaongeza hawa Maafisa ili tuweze kuwa na *out reach* kubwa zaidi na waajiri wengi kwa hilo wanalifahamu, na ndio maana wanakuwa wajanja katika kutokutoa mikataba kwa sababu wanajua kwamba mikono ya serikali bado haijawa mipana sana kwa kuwafikia.

Kuhusu kupokea orodha ya kampuni ambazo hazitoi mikataba, hilo tunalipokea lakini vile vile sasa hivi tunaandaa zoezi maalumu la kufanya *labor audit* kwa maana ya kuwa angalau kuanzisha *task force* ambayo itakuwa inapita katika hayo maeneo na kuhakikisha kwamba suala la mikataba linasimamiwa vizuri. Kwa hiyo, hiyo *task force* ipo ni *multi central task force* ambayo tayari imeshaanza kufanya kazi yake.

**Nam. 44**

**Ujenzi wa Tangi la Maji la Mtambile**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha** – Aliuliza:

Katika Baraza lililopita niliwahi kuuliza swali kuhusu ujenzi wa tangi la maji safi liliopo katika Jimbo la Mtambile na kujibiwa ujenzi huo utafanyika. Pamoja na kuletwa vifaa vya ujenzi wa tangi hilo, lakini hadi leo ujenzi wa tangi hilo haujafanyika.

(a) Je, ni lini ujenzi huo utafanyika.

(b) Je, ni lini ujenzi huo utakamilika na kuwatatulia changamoto ya kukosa maji wananchi wa maeneo hayo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile swali lake Nam. 44 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu, kupitia Mamlaka ya Maji, ilidhamiria kulifanyia matengenezo tangi la Mtambile, ila kwa sasa tangu hilo haliwezi kutengenezeka tena kutokana na hali ya uchakavu mkubwa wa tangi hilo. Hivyo, Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) imepanga kujenga tangi jipya katika Jimbo la Mtambile ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Jimbo hilo.

(c) Mhe. Naibu Spika, kuna mradi unatarajiwa kuchukua miezi 18 hadi kukamilika kwake. Hivyo, wizara inawaomba wananchi wa Jimbo la Mtambile kuendelea kuvuta subira kwa kuendelea kutumia maji yanayopelekwa katika maeneo husika kwa njia ya moja kwa moja *(Direct pumping)* hadi ujenzi wa tangi hilo utakapokamilika.

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ilionekana kama hii hali ya subira katika kuuliza maswali yangu imekuwa ni ndio jibu, juzi niliambiwa hivyo hivyo utasubiri na leo Mheshimiwa ananiambia nisubiri vile vile. Lakini katika awamu mbili zilizopita katika Baraza hili hili niliuliza swali hili la tangi nikaambiwa kumebakia kitu kimoja tu ni dawa yaani vifaa vyote vishakamilika, awamu zimepita mara mbili na hii ni awamu nyengine mpya ya Awamu ya Nane. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri tu ni kitu gani kilichokuwa hakijakamilika kwenye tangi hili la Mtambile.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa kutokana na swali mama. Mheshimiwa tangi hili baada ya kulifanyia utafiti hiyo dawa ambayo ilisemwa katika tangi hilo hata ikiwekwa hilo tangi haliwezi tena kufanya kazi, kwa sababu limeshachakaa na limeshapitwa na muda. Mbadala uliokuwepo Mheshimiwa ni kujenga tangi jengine jipya la kisasa sio lile tangi la mabati kama ilivyozoeleka, matangi haya yanaonekana yamepitwa na muda na hayawezi tena kufanya kazi kwa ufanisi.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri mwanana yenye kuakisi kile ambacho tunakiuliza. Pamoja na majibu mazuri hayo nina swali moja la nyongeza, Mhe. Waziri wakati unajibu swali la msingi linalohusiana na tangi la maji. Mimi swali langu ni kuwa serikali ina mpango gani wa kukarabati kadhia kama hii ya matangi, mimi jimboni kwangu tangi la Ukongoroni, Marumbi pamoja na udogo wa tangi la Chwaka. Kadhia hii kwa maana ya kwamba itakuwa endelevu, serikali ina mpango gani kwa ujumla juu ya suala zima la kubadilisha matangi ambayo mabovu au matangi ambayo madogo yanayoshindwa kutoa huduma ya maji kama yalivyo matarajio ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Nashukuru Mhe. Naibu Spika, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Wananchi Chwaka kwa swali lake zuri.

Mhe. Naibu Spika, mpango wa serikali ni kuyafanyia ukarabati matangi yote ambayo yanaweza yakafanyika ukarabati, na yale ambayo hayawezi kufanyiwa ukarabati Mhe. Naibu Spika, tuna mpango wa kujenga matangi mengine mapya ya kisasa ili kukidhi haja ya usambazaji wa maji na upatikanaji wa huduma hii muhimu kwa wananchi wote wa Zanzibar.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, kama tunavyojua kuna matangi ambayo tangu mwaka 1971 tangi hilo lipo Kironjo. Je, una mpango gani wa kujenga tangi jengine eneo lile la Kironjo.

Mhe. Waziri, Maziwa ng'ombe kuna tangi ambalo limejengwa kwa kuelekeza maji Kiuyu Maziwa ng'ombe, tangi lile naona halifanyi kazi. Je, una mpango gani wa kulifanyia marekebisho

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru lakini majibu yangu yatafanana na yale ambayo yamepita kwamba, yale matangi yote ambayo tumeona hayafai kwa sasa na hayana tija kwenye usambazaji wa huduma hii muhimu ambao pia unapelekea upotevu mkubwa wa maji, na kukosesha wananchi huduma. Tuna mpango wa kuyaondoa na kuweka matangi mapya ya kisasa yatakayokidhi haja ya usambazaji wa huduma hii ili kuweza kudhibiti upotevu wa maji na kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama kwa uhakika zaidi

**Nam. 23**

**Udhalilishaji wa Wanafunzi katika Skuli**

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis (Kny. Mhe. Salma Mussa Bilal):–** Aliuliza:

Pamoja na jitihada za serikali kupiga vita suala la udhalilishaji kwa nguvu zake zote, sasa limeibuka suala la udhalilishaji na ulawiti wa wanafunzi wenyewe kwa wenyewe katika skuli na hata nje ya skuli (mitaani).

(a) Je, Serikali inalitambua suala hilo.

(b) Kama inalitambua suala hilo, Wizara imechukua hatua gani.

(c) Je, Wizara imefanya utafiti kujua chanzo na ukubwa wa tatizo hilo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):-** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua uwepo wa suala la udhalilishaji na ulawiti wa wanafunzi katika skuli na hata nje ya skuli (mitaani).

(b) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imechukua hatua mbali mbali katika kukabiliana na suala hili. Miongoni mwa hatua ilizochukuwa ni kuzifikisha kesi hizi kituo cha Polisi kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria, kutoa elimu kwa wanafunzi kuhusiana na masuala ya udhalilishaji, kuweka walimu wa ushauri nasaha katika skuli

kusaidia kuwanasihi wanafunzi katika kujiepusha na maswala mbalimbali yanayokwenda kinyume na maadili yakiwemo ya udhalilishaji, kushirikisha wazazi kufanya vikao nao vya kuhamasisha kufuatilia mwenendo wa watoto wao.

(c) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya utafiti kujua chanzo na ukubwa wa tatizo la udhalilishaji katika mwaka 2016. Utafiti huu umefanyika baada ya kugundua kwamba tatizo la udhalilishaji na ulawiti linaongezeka kutokana na takwimu zinazotolewa. Katika utafiti huo wizara imegundua kuwa udhalilishaji unachangiwa zaidi na kutofuatwa kikamilifu kwa Kanuni ya Nidhamu za Wanafunzi za Mwaka 1996, kuachana kwa wanandoa, wazazi na matumizi mabaya ya simu na mitandao. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Nimpongeze Mhe. Waziri lakini hili ni suala la kusikitisha kwa watoto wetu. Mhe. Waziri, naomba nikuulize swali moja la nyongeza, tunakumbuka miaka ya nyuma kulikuwa na utaratibu kwenye skuli zetu kuletewa madaktari wa kutupima wanafunzi ili kujua tatizo ni nini la wanafunzi. Je, una mpango gani utaratibu huu kuurejesha skuli.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nimjibu Mhe. Bihindi Hamad Khamis Mwakilishi wa viti maalum Mkoa wa Kaskazini Pemba swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli suala hili lilikuwepo nakubaliana na yeye lakini bado linaendelea sio kwamba halipo moja kwa moja ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto inakuwa inafanya utaratibu ya kuwapima wanafunzi katika maradhi na mambo mbali mbali. Wanafunzi wanafanyiwa vipimo masuala ya meno, macho na masuala mengine yakiwemo kutizama vile vile afya zao. Lakini kutokana na ukubwa wa ada za skuli zetu vile vile kutokana na ugatuzi ambao umetokezea suala la ngazi ya maandalizi na msingi zaidi imewekwa katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni Skuli za Sekondari, lakini zoezi ambalo bado linaendelea kufanyika kwa kushirikiana pamoja katika wizara hizo zote na kwa vijana wetu wanafanyiwa hivyo vipimo. Nakushukuru Mheshimiwa.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Mhe. Waziri yupo tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kushirikiana pamoja na wizara inayohusiana na Idara Maalum ya Serikali katika kuzibaini taasisi au *NGOs* Taasisi Zisizo za Kiserikali ambazo kwa namna moja ama nyengine zinadhamini vitendo hivi vya udhalilishaji kwa makusudi mazima ili watuletee ripoti ya uwazi na ukweli kabisa katika kubaini tatizo hili.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, sisi Wizara ya Elimu ni serikali, Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ni serikali na taasisi nyengine za serikali tupo tayari kwa sababu ni wajibu wetu kuwasimamia vijana wa Kizanzibari. Kwa hivyo, niseme kwamba serikali tuko tayari kuona kwamba tunazibaini au pengine zinajulikana sijui, lakini kama watu wanazijua basi tutashirikiana na serikali na vyombo vyake husika. Nimesema hivyo kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hata ikienda haina mamlaka ya kumkamata mtu kwa sababu wao hawana vyombo vile vya ulinzi, lakini maana yake ile kushirikiana na taasisi zote ambazo zinahusika basi tuko tayari kushirikiana kuona kwamba tunapiga vita lakini tunavikamata vyombo vyote ambavyo vinahusika na kutudhalilishia vijana wetu. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba nimuulize swali la nyongeza.

(a) Wizara ya Elimu wanasema kwamba miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuzifikisha kesi hizi katika Kituo cha Polisi kwa ajili ya kuchukua hatua zaidi. Nataka kumuuliza je, ni kesi ngapi ambazo zimefikishwa katika Vituo vya Polisi za wanafunzi ambao wamedhalilishwa. Lakini pia ni hatua gani ambazo zimechukuliwa.

(b) Wanasema kwamba wizara wamefanya utafiti wa kujua chanzo cha ukubwa wa tatizo hili la udhalilishaji katika mwaka wa 2016. Pia wamekiri kwamba wamesema tatizo hili la ulawiti limeongezeka kutokana na takwimu zilizotolewa. Nilitaka kujua kwamba kwa mwaka 2016 – 2020 tatizo hili limeongezeka kwa kiasi gani. Ni kesi ngapi ambazo zilionekana lakini pia mpaka sasa zimefikia ngapi. Ahsante mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, suala la Mhe. Asha Abdalla Mussa ametaka kujua takwimu ni kesi ngapi, ningemuomba sana kwa sauala la takwimu nimletee kwa maandishi. Katika takwimu ambazo tutaleta maana yake nitawaelezea vile vile kwamba ni kwa kiwango gani kesi hizi zimeongezeka ama zimeweza kupungua, kwa sababu yote ni masuala ambayo yanaendana na hizo hesabu.

(b) Lakini hatua gani ambazo zimechukuliwa vile vile kwamba nitaomba nitakapojibukwa maandishi hizo takwimu basi na hatua ambazo zimechukuliwa nitaomba vile vile nimfikishie. Lakini naomba tu kumwambia kwamba sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunakuwa tunafanya kazi za kushirikiana na taasisi nyengine sio sisi peke yetu. Kwa hivyo, sisi wizara tunapobaini kesi kama hizi tunazifikisha kama ambavyo tumeeleza katika vyombo ambavyo vinahusika na masuala ya sheria na kuchukua haki zake mkondo unachukuliwa. Kwa hivyo, kwa mujibu wa sheria kwamba kesi ile inakwenda kwa mujibu wa sheria kama ambavyo inaeleza. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 68**

**Wawekezaji Binafsi katika Sekta ya Elimu Zanzibar**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum-** Aliuliza:

Serikali imeruhusu wawekezaji binafsi katika sekta ya elimu hapa Zanzibar, ambao wamesaidia kwa kiasi kikubwa sana kunyanyua kiwango cha elimu.

(a) Je, ni masharti gani ambayo serikali imewawekea Wawekezaji wa Sekta ya Elimu wa Kimataifa wanaokuja kufanya uwekezaji katika Sekta ya Elimu hapa Zanzibar.

(b) Je, mambo gani hasa serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikiyaangalia wakati wa ufuatiliaji wa uhakiki wa uwekezaji katika elimu, ili kuhakikisha ufanisi na tija vinapatikana kwa jamii ya watu wa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): –** Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, masharti ambayo serikali imewawekea Wawekezaji wa Sekta ya Elimu wa Kimataifa wanaokuja kufanya uwekezaji katika Sekta ya Elimu hapa Zanzibar ni pamoja na Kufuata Sera ya Elimu ya mwaka 2006 na Sheria ya Elimu Nambari 6 ya 1982, lakini vile vile kufuata Kanuni na Miongozo ya Elimu, pia kufuata mwongozo wa majengo ya skuli uliotayarishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, vile vile kukata vibali vya ukaazi na vibali vya kufanya kazi nchini, sambamba na kukata leseni ya kufundishia kwa walimu wote wa skuli husika.

(b) Mambo ambayo serikali kupitia Wizara ya Elimu imekuwa ikiyaangalia wakati wa ufuatiliaji wa uhakiki wa uwekezaji katika elimu ili kuhakikisha ufanisi na tija vinapatikana kwa jamii ya watu wa Zanzibar ni pamoja na:

1. Kuwekeza katika maeneo ambayo yana uhaba wa skuli.
2. Kuwa na walimu wenye sifa za kufundisha katika skuli wanazozifungua.
3. Utozaji wa Ada.
4. Uwezo wa kutoa elimu bora.
5. Uwezo wa kufuata Sera ya Elimu Sheria ya Elimu namba 4 ya mwaka 1982.

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake. Nina maswali ya nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, uwekezaji katika elimu unafuata *principle* za uwekezaji kwa Zanzibar katika sekta nyengine. Je Mhe. Waziri anafahamu kuwa katika uwekezaji huu kwenye elimu hususan unaotokea wa kimataifa kwamba si wazawa wengi wapo katika *management* hata kama hizo sifa zinapatikana hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, swali la pili, wawekezaji wa kimaita wanapokuja hapa pamoja na mambo mengine, kuna vitu vipya ambavyo vinaingia. Kwa mfano kuna wawekezaji wamekuja kuwekeza hapa katika elimu lakini wanatoka nchi moja, huko wanakotoka ni nchi moja na inawezekana kabisa huko nchini kwao wanakuwa na tofauti zao, iwe za kisiasa *either* katika uwekezaji, lakini inasababisha hizi skuli ambazo wawekezaji wanatoka nchi moja lakini wana *operate* skuli tofauti, inakuwa kuna *conflict* baina ya skuli moja na skuli nyengine, *in such a way* kwamba anaetoka skuli hii akienda kupata *service* katika skuli nyengine kunakuwa kuna ugomvi baina ya hizi skuli.

Je Mhe. Waziri kwanza analifahamu hili. lakini la pili Je *context* kama hii kwa nini haimo katika miongozo ama masharti ambayo serikali inaiweka katika uwekezaji kwenye elimu. Kwa sababu unaathir sana *service delivery* kwenye elimu hapa nyumbani. Ahsante nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia uwekezaji ni kwamba uwekezaji hauko moja kwa moja kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bali kwa sasa ipo katika Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji. Sasa kwa mfano inapokuja suala la uwekezaji wa *international school*, Wizara ya Elimu ambacho inaingia kutizama pale ni zile sifa na miongozo ambayo inahusiana na masuala ya elimu. Lakini uwekezaji kwa ujumla wake unafuata misingi yote ambayo muwekezaji mwengine anapaswa kuifuata.

Kwa hivyo, misingi hiyo, kwa sababu si Waziri husika ya hiyo *sector* moja kwa moja, kwa hiyo nadhani Waziri husika mwenyewe anajua zaidi misingi ambayo wanafuata kwa wawekezaji wengine wa kimataifa wanapokuja nchini. Lakini kimoja nnachokielewa ni kwamba kwa walimu hawa, wanakuweko walimu wa kigeni. Kwa sababu nakumbuka tulijibu swali hili katika maswali yetu yaliyopita, ni kwamba wawekezaji katika skuli ya kimataifa kama kwa Zanzibar tuseme inayotambulika hasa ni skuli moja, na katika skuli hii kuna wanafunzi ambao wanasoma katoka mataifa mbali mbali kutokana na wazazi wao wapo Zanzibar kutokana na majukumu yao ya kikazi ama kibalozi na masuala mengine.

Kwa hiyo, ina maana kwa msingi huo hata baadhi ya walimu wake wako ambao na wao si wazawa wa Kizanzibari ina maana inawezekana miongoni mwao labda ni wale wake wa wale viongozi wa kibalozi na kadhalika.

Kwa hiyo, masuala zaidi ya uwekezaji basi nitamuomba sana Mhe. Saada Mkuya Salum, hilo tilielekeze kwa waziri ambae anahusika na masuala ya uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, swali la pili ambalo ameliuliza tofauti ya wawekezaji. Niseme kwamba kwa Wizara ya Elimu hatuna kesi mkononi ambayo imeletwa labda kulalamika kwa mfano skuli x kuilalamika skuli y moja kwa moja na ikaleta athari kwenye elimu yetu. Kama tutapata kesi kama hiyo basi tutafuatilila na tuone ambavyo tunaweza kuimaliza na kuondosha hiyo migogoro. Lakini nnavyozungumza sasa kesi hiyo moja kwa moja hatuna, ambayo imeripotiwa kwamba kuna skuli wawekezaji wake wanatofautiana kutokana na siasa au masuala mengine na ikapelekea athari ya moja kwa moja. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Mimi ningependa kuuliza kuna hizi skuli nyingi za *private* wanafunzi wakifikia *form II* akiwa hajafanya vizuri katika mitihani yake, huambiwa akatafute skuli nyengine ambapo huwapa usumbufu mkubwa watoto wetu.

Sasa napenda nimuulize Mhe. Waziri je kufanya suala hilo si kukiuka muongozo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kwa mujibu wa miongozo yetu skuli kama hii haipaswi kufanya kitu kama hichi na kumuondosha huyo mtoto. Inapobanika, maana yake yaje maalalamiko, na yameshawahi kuja malalamiko kama kwamba kuna skuli x, wanafunzi kwa mujibu wao wanasema kwamba hawakutimiza vigezo wakawaondosha wote na wizara iliingia kati na kuwaambia kwamba wanafunzi hao lazima waendelee kusoma katika skuli yao.

Kwa hiyo, inapokuja tatizo kama hili, basi wizara inakuwa inasimama katika kuona kwamba wanafunzi wale wanaendelea kupata haki yao. Lakini kama mzazi mwenyewe ataamua kumtoa mtoto wake, hapo tena sisi wizara inakuwa hatuna la kumlazimisha. Lakini kama haki yake basi tunataka kwamba aendelee kubaki kupata haki yake katika skuli hiyo. Ahsante sana mheshimiwa.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Tumeona huko mitaani watu wengi wanafungua mashule na wanapenda kuziita shule zao *x, y international school whatever*. Lakini ukiziangalia hizo skuli hazina sifa yoyote ya kuwa *international* kwa maana ya mahitaji na vifaa. Je wizara kuna kanuni au sheria zinazoratibu matumizi ya majina kwa skuli pale ambapo watu wanafungua maskuli.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya amali, napenda kumjibu Mhe. Omar Said Shaaban swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, alichokizungumza mheshimiwa ni kweli kuna skuli *x,y, z international school* na zipo nyingi na tunazielewa. Katika kuliona hilo, ni kwmba wizara imeendaa miongozo maaluma na katika kuandaa miongozo hiyo ni kwamba inakwenda kufanya ukaguzi kujiridhisha

na inawawepekea katika zile skuli wajaze na itakapoona kwamba kweli imekidhi vigezo, basi itaendelea kutumia hilo jina. Lakini endapo itaonekana kwamba haijakidhi hivyo vigezo vya kuiita *international school* basi ni kwamba tutawaomba wenzetu Baraza la Mitihani kwamba skuli hiyo jina lake tulirekebishe na ile *international* iweze kuondoka. Ni hilo, nakushukuru sana mheshimiwa.

**Nam. 11**

**Ukusanyaji Mapato Katika Mamlaka ya Usafiri**

**Mhe. Mussa Foum Mussa** – Aliuliza:-

Mamlaka ya Usafiri na Usalama barabarani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika malengo ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 3,400,585,000/- kupitia vyanzo vyake vya mapato.

Je, suala hilo limefikia hatua gani za utekelezaji hadi sasa.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Mamlaka ya Usafiri na Usalama barabarani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS. 3,400,585,000/- kupitia vyanzo vyake vya mapato.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa suala hilo kutoka Julai hadi Disemba, 2020 Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tzs. 1,744,915,000 na imeweza kukusanya jumla ya TZS. 1,248,014,700/- ikiwa ni sawa na asilimia 72% ya makadirio ya kipindi hicho.

Kutokana na hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Mamlaka za kuhakikisha mapato yote yanayotokana na vyanzo vya Mamlaka yanakusanywa pamoja na kuondoa mianya yote inayoashiria kuvuja kwa mapato, tunategemea kwamba Mamlaka itafikia lengo hilo la ukusanyaji kama lilivyopangwa. Ahsante mheshimiwa.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuolize swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri ametueleza hapa kwamba lengo la miezi 6 ilikuwa ni shilingi bilioni moja, milioni mia nne na arubaini na nne, laki tisa na kumi na tano, lakini lengo hilo hakulifikia, akakusanya bilioni moja, milioni mia mbili na arubaini nane, kumi na nne elfu na mia saba. Kwa muda wa miezi 6. Je namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa lengo kuu la mwaka bado halijafikiwa na muda uliobakia ni mdogo, Je ana mikakati gani kabambe na kuonesha kwamba lengo hilo litafikiwa kwa muda uliobakia.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo, kwa operesheni ambazo tunazifanya za mara kwa mara za magari tunatarijia kufikia hilo lengo ambalo tumefikia. Kwa sababu kwa kipindi cha Januari tumeongeza mapato kuliko huko nyuma. Kwa hivyo, tunarajia kufikia kutokana na operesheni ambazo tunazifanya mara kwa mara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, ili afikie lengo ni watu kufanya makosa barabarani akapata hiyo faida yenyewe. Mhe. Waziri katika bajeti yake hiyo imeonekana sasa hivi kuna tabia sana ya kuchukuliwa madereva na kondakta kuwekwa ndani kwa masaa 24, siku ya pili kupelekwa mahakamani. Je haoni sasa mfumo huu ukabadilika na kuweka mashine na faini ya papo kwa papo ili kuhakikisha kwamba faini hizi zinatolewa na pesa inakwenda moja kwa moja katika mfuko mkuu wa serikali.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali la nyongeza kama ifuatavyo. Tumeona ni kweli kuna tatizo la kumuangalia mtu kwa kawaida. Kwa hivyo, hivi sasa tuko katika utaratibu huu kwa kutafuta mashine na kufanya kazi kwa mashine. Na utaratibu huo tutaanza hivi karibuni. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake maziri na mwanana.

Mhe. Naibu Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri, kwa vile vyombo vya usalama barabarani vina tabia ya kuvishika vyombo na kuvipandisha juu, yaani kuviweka juu kama wamevizuia. Kufanya suala hili kiutaratibu tunaita ni *ultra vires* kwamba wamekwenda *beyond* kwenye mamlaka yao. Je haona sasa kwamba chombo sicho kulichofanya kosa, bali mwenye chombo ndio aliefanya kosa, kwa nini sasa hawasimamii makosa yale kwa faini ya yule mwenye kufanya kosa, bila kukipandisha chombo kama kimefanya kosa. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shaaban Hassan Kaduara swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Najua mamlaka inafanyakazi kisheria, sasa kama inakiuka utaratibu wa kisheria hilo ni suala jengine na tutalifuatilia hilo swali. Lakini najua inafanya kazi yake kisheria na ina sheria yake ambayo inafanyia kazi. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi)*

**Nam. 32**

**Ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri**

**Mhe. Hassan Hamad Omar** – Aliuliza:-

Suala la ujenzi wa bandari ya Mpiga duri limekuwa la muda mrefu.

a) Je, ni lini ujenzi utaanza na lini unatarajia kukamilika.

b) Je, bandari ikikamilika na kuanza kutumika, itaondoa kero gani na itasaidia shughuli zipi za kimaendeleo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake kama ifuatavyo, kabla ya kujibu swale lake namba 32 naomba kwanza kutoa maelezo.

Mhe. Naibu Spika, katika eneo la Mpigaduri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia katika mradi wa ujenzi wa bandari shirikishi ya uvuvi ambao ni hatua nyengine ya mabadiliko ya kiuchumi. Mradi ambao serikali ina matarajio makubwa ya kuongeza mapato pamoja na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mhe. Naibu Spika, mradi wa bandari ya uvuvi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo.

1) Ujenzi wa maegesho ya meli za uvuvi.
2) Ununuzi wa meli za uvuvi wa bahari kuu.
3) Ujenzi wa chelezo cha kujengea na kutengenezea meli.
4) Ujenzi na kiwanda cha kutengenezea boti ndogo ndogo.
5) Ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea nyavu na dhana za uvuvi.
6) Ujenzi wa kiwanda cha kusindika minofu ya samaki.
7) Ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea mbolea inayotokana na mabaki ya samaki.
8) Ujenzi wa maghala ya mafriji.
9) Ujenzi wa soko la mnada wa samaki.
10) Pamoja na ujenzi wa chuo cha kufundishia uvuvi na ubaharia.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi huu utafanyika kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na makampuni matatu ya uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu utakuwa kwa awamu ya kwanza, kufanya upembuzi yakinifu. Baadae awamu ya pili ni utiaji wa saini ya mkataba wa ujenzi.

Kwa hatua ya sasa hati ya makubaliano imeshatiwa saini na ambako mradi huu upo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Sasa naendelea kumjibu swali lake, ilikuwa ni maelezo tu yale.

Mhe. Naibu Spika, katika suala namba 32 najibu kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba hapo awali Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga Bandari ya mizigo katika eneo la Mpigaduri. Hata hivyo, imeonekana kwamba Mangapwani ni sehemu muafaka zaidi ya kujenga bandari hiyo kutokana na maumbile, ukubwa wa eneo pamoja mandhari ya eneo lenyewe. Tayari, Serikali imeshatiliana saini na Mamlaka ya uwekezaji wa Omani kwa ajili ya kutayarishwa mpango mkuu, *(master plan)* ya ujenzi wa bandari hiyo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, namuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri dhamira ya kujengwa bandari ya Mpigaduri si ya mizigo ili

kupunguza usumbufu ulio katika Bandari ya Malindi. Sasa hivi kule Mwangapwani kumeainishwa kujengwa bandari ya uvuvi. Je bandari hii ya uvuvi na kushusha mizigo zote zitajengwa Mangapwani.

Vile vile, kwa sababu suala hili ni la muda mrefu, matarajio ya kuanza bandari hiyo ya kushusha mizogo itakuwa lini na itamaliza lini. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa upande wa Bandari ya Mangapwani, sasa hivi inafanyika *master plan, feasilibity study,* kwa hivyo, kwa muda wa miezi 6 itakuwa tayari imeshakamilika hiyo *feasibility study* na baada ya hapo serikali itayaalika makampuni mbali mbali kuja kutengeneza hiyo bandari.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mradi huu una tija na faida kubwa kwa maslahi ya Taifa la Zanzibar, je, Mhe. Waziri kupitia wizara yake yupo tayari kuunda kikosi kazi maalum *Task Force,* kikosi kazi hiki kitakuwa kinaundwa na vikosi vya Usalama, Ulinzi pamoja na *ZAECA* ambapo watakuwa wanafuatilia maendeleo ya mradi huu hatua ya mwanzo, hatua ya kati na hatua ya mwisho na kila hatua itakayoipitiwa kuwachukuliwa nidhamu wale watakaokuwa wanarudisha nyuma mradi huu kuwaekea vikazo usiendelee wako tayari katika hatua hiyo, ili kuona mradi huu sasa unawanufaisha wananchi wa Zanzibar na unakamilika kwa mujibu wa vile ambavyo umetabiriwa kuwa hivyo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba suala hili nilipeleke kwenye serikali ambapo bado mradi huu uko kwenye serikali. Kwa hivyo, naomba nilipeleka katika Serikali Kuu wao watapata kulijibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante nimeoma mikono ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu. Kwa hiyo, tuanze na Mheshimiwa na baadae tuendelee na Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Waziri naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema Mhe. Waziri hapa tuna bandari mbili tuna Bandari ya Mangapwani ambayo itahusika zaidi na mizingo lakini pia na *Oil and Gas* na pia kutakuwa na Chelezo na hiyo tayari imeshasainiwa hati ya makubaliano kunafanyika *feasibility study* hivi sasa na kampuni inayofanya *feasibility study* ameitaja kama ni *Oman Investment Authority*.

Lakini Bandari ya Mpiga Duri nayo tayari hati ya makubaliano imeshasainiwa na Kampuni inayoitwa *Tanjen Intercom* kazi hii itafanyika ndani ya miezi sita na tayari hati imeshasainiwa sasa tusubiri *feasibility study* hizo kumalizika. Mara baada ya kumalizika itaainishwa miradi ambayo itatekelezwa kwa mfano kwenye hati hii ya Mpiga Duri kuna miradi karibu kumi

inafanyiwa *feasibility study*. Baada ya kufanyika *feasibility study* hiyo serikali itaelekezwa na feasibility study hizo kwenye miradi ya uwekazaji. Kwa hivyo, kwa sasa hakuna haja ya kuunda kikosi kazi. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi una lolote.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Naibu Spika, jibu la Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais linatosha Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa alikuwa Mhe. Waziri pale amefanya jambo ambalo nilikuwa nataka kujaribu kushauri mawaziri na nafahamu kwamba mawaziri wengine ni wapya. Lakini mara nyingi sana maswali ambayo yanakuja hapa ya msingi Waheshimiwa Mawaziri wanayajibu vizuri sana.

Sasa kuna maswali ambayo yanakuja ya nyongeza yale ya mchepuko yaani yanachepuka yanatoka kwenye ile *line* ya lile suala la msingi. Mara nyingi sana kwa maana hiyo kwa sababu hapa tuna serikali na kunatakiwa kuwepo kwa *collective responsibility* na pengine waziri fulani lile suala analijua vizuri zaidi kulijibu kwa hiyo ningeomba sana liwepo hilo kwa sababu kuna baadhi na maswala huko nyuma ni hili ambalo Mhe. Rais amefanya vizuri Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amelifanya vizuri sana.

Lakini kuna maswala mengine ilikuwa ni Waziri mwengine anaweza kujitokeza na kusema pamoja na majibu mazuri lakini kwa sababu yanakuhusu wewe vile vile basi na wewe unaweza kuchangia katika majibu hayo na kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe mara nyingi sana maswali ambayo wanayaleta hapa ni maswali yanayotoka kwa wananchi na wananchi nao wanatusikiliza na wanataka majibu sahihi.

Kwa hiyo, ningeomba sana Waheshimiwa Mawaziri muwe na *collective responsibility* kwenye masuala hayo ambayo yanajibiwa hapa na Waheshimiwa Wajumbe.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa tunaendelea katibu.

## TAARIFA YA SERIKALI

### Hotuba ya Muelekeo wa hali ya Uchumi Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 - 2023/2024

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa majadiliano yanaendelea nina wachangiaji wanafika ishirini. Lakini ratiba yetu inatwambia tunamaliza leo kwa maana kwamba bado tuna fursa nzuri kwa wachangiaji wote wanaweza kuchangia kwa sababu tutarudi tena jioni. Basi nianze na Mhe. Nadir Abdullatif Yusuf baada ya Mhe. Nadir Abdullatif atafuata Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na baada ya hapo atafuata Mhe. Ameir Abdalla Ameir.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** *"Bismilah Rahman Rahim"* Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii naomba nichangie Hotuba ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi wa Mpango wa Maendeleo wa Bajeti kwa mwaka 2021/2022 – 2023/2024 ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kuanza kuchangia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha huu mpango wa Maendeleo aliouleta ni mpango ambao mzuri sana na kitabu kidogo lakini chenye maneno ya kufahamika na wengi wao hata kama hawana uzoefu lakini jinsi ulivyokitengeneza ataweza kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu ambapo tulivyoanza na serikali yetu hii ya awamu ya nane tumeanza vizuri tumpongeze Mhe. Rais Dr. Hussein Ali Hassan Mwinyi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamu wa kwanza na wa Pili jembe langu Mhe. Hemed Sueleiman Abdulla naamini sana kwa mwenendo huu na hotuba hii ya Muelekeo wa Bajeti Mwenyezi Mungu akitujaalia tufike pale tunapotaka na kama ilivyo basi Zanzibar sasa mara hii yatatokea maajabu mengi kwenye maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningemshauri Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ni Waziri wa Fedha kijana ameanza vizuri na tunaelekea pazuri. Ningemuomba sana baadhi ya wakati kwa kuwa humu ndani wamo Mawaziri wa Fedha wastaafu na wazuri na wote walipokuwa wakiendesha wizara zao Mhe. Dr. Khalid Salum Mohamed na Mhe. Dr. Saada Salum Mkuya wamefanya kazi zao vizuri na hawakufeli wakati walipokuwa wakiendesha Wizara za Fedha za Muungano lakini na Dr. Khalid Salum aliyekuwa Waziri wa Fedha kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye *page* 25 kwa kweli mapato ya ndani yanasema kwa mwaka 2021-2022 bilioni 1,105.5 Halafu ukienda mwaka 2022 bilioni 1,286.2 na 2023-2024 bilioni 1,422.0. Hapa inaonesha dhahiri kwamba tunapokwenda kwenye *chapter* ya pili Msaada wa Bajeti tunakwenda kwenye *chapter* ya tatu Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2122 ni 16.2 *billion* halafu 2022-2023 ni 16.5 *billion* na 2023-2024 ni 16.9 *billion*. Hapa Mhe. Waziri wa Fedha naona imepanda kidogo tu kila mwaka kwa sababu kwenye masuala ya Mapato wa ndani.

Ningeomba sana mjitahidi kwenye mapato ya hapa pia yawe yanaongezeka vile vile na isiwe yanapanda hivi kidogo kidogo. Lakini kwenye mkopo wa ndani tumeona mwaka wa kwanza bilioni hamsini mara ya pili mwaka 2022 bilioni hamisini lakini mwaka 2324 bilioni arubaini imeshuka kwa maana wamepunguza kiwango cha mkopo wa ndani.

Hapa Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla kwa mujibu wa hesabu ya mwaka 2122 jumla ni trilioni 1,506.2 lakini ukijumlisha sasa ndani yake kuna mkopo na ruzuku za bilioni 332.5 na Mfuko wa pamoja wa wafadhili bilioni 2.0.

Mhe. Naibu Spika, ningemshauri sana Mhe. Waziri wa Fedha naamini mwanzo siku zote ni mgumu lakini kwetu sisi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu utakuwa ni rahisi. Sasa popote tunapokwenda mbele tungejitahidi sana tukapunguza masuala ya mikopo na zuruku tusiyategemee sana kwa sababu kama unavyofahamu mikopo na ruzuku zinatokana na maeneo mengine na nchi nyengine na nchi nyengine wakati mwengine haziaminiki wanapokuwa wana

jambo lao wakati wowote wanaweza wakazuia hivi vitu na wakakutetemesha katika masuala yetu ya uchumi.

Sasa ningeshauri sana Wizara ya Fedha tungekuwa tunajikita sana kwenye kutegemea kipato ambacho tunaingiza wenyewe nchini ambacho tunachokiona hapa kwa kujibu wa *draft* karibu takribani asilimia sabini au sitini na saba pointi kidogo ndio tunaingiza wenyewe na nyengine zilizobakia tunategemea kwa wafadhili au ruzuku kama ulivyosema.

Tumeona miaka ya nyuma kwamba nchi nyingi tunapofanya maamuzi ya kitu chochote wakati mwengine serikali zinatugomea na zinatuonesha jeuri kwa sababu tunazitegemea. Lakini kwa hali ya uchumi unavyokwenda na muelekeo huu mliouleta kwa kweli una kila kitu. Mimi binafsi sijui hata nichangie nini kwa sababu kila mlichokiandika humu kila sehemu *page* unayokwenda kuanzia *page* ya 21 hadi 25 ni mambo ni mazuri na mambo ni makubwa na Mwenyezi Mungu akijaalia iwe hivi kama ilivyopangwa ndivyo ilivyo, basi nchi yetu sasa hatutotegemea tena ruzuku wala hatutomtegemea mtu alete kitu chake na bali tutajiendesha wenyewe kwa mujibu wa kipato chetu cha ndani na *income* yetu ambayo tunapata katika vianzio tafauti.

Mhe. Naibu Spika, kuna vitu muhimu humu mmevieleza humu kwenye *page* ya 21 Ujezi wa Bandari ya Mangapwani pamoja na masuala ya Uvuvi, Ujenzi wa Kiwanja cha ndege Pemba, Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Mpigaduri, Ujenzi wa Daraja, Ujenzi wa Barabara kilomita mia moja na thalathini na tano masuala ya *Industrial Park* masuala ya maji, masuala ya *Airport* ya Zanzibar, masuala ya Utalii.

Mhe. Naibu Spika, mimi niongelee kwa pamoja hivi vitu, siku zote nchi katika wananchi wanahitaji vitu fulani ambavyo ni muhimu kwao afya na humu imetajwa mahospitali makubwa na naamini zitakapomaliza matibabu Zanzibar yatakuwa mazuri kwa Wazanzibari pamoja na wageni.

Lakini vile vile suala la elimu humu limo na ndio tunataka tuwape elimu wananchi wetu ili waje waiendeshe Zanzibar bila ya kutegemea wageni. Sasa hivi mmeona kwamba wageni wengi wanaajiriwa kwa sababu kuna baadhi ya nafasi Wazanzibari bado hatujaziweza lakini pindipo tutakapokuwa tuko wengi na tumesomea vile vitu na tumebobea basi wageni itabidi tuwaweke kando kama wanavyoweka kando nchi nyengine na kuwapa vipaumbele wazalendo.

Mhe. Naibu Spika, ndani kumezungumza masuala ya maji, masuala ya umeme, masuala ya barabara, masuala ya elimu na masuala ya afya na masuala ya ajira. Vitu sita hivi kwa wananchi kwenye nchi yoyote vikiwepo kwa uzuri na kwa ufasaha, basi nchi haitetereki na nchi itafaidika na matunda yake.

Nimuombe sana Mwenyezi Mungu aijaalie serikali hii tunayofanya nayo kazi na imeonesha upendo sana kwa wananchi wote kwa ujumla pamoja na sisi viongozi wa Baraza la Wawakilishi wafanikiwe na mipango hii na waweze kupeleka mbele gurudumu hili na mimi nawaombea wote hakuna mkamilifu bali nawaombea wote wafanikiwe tuweze kufanyakazi hii pamoja.

Mhe. Naibu Spika, jana nimeona kuna ndege takribani saba *Airport*, katika jambo kubwa ambalo tunalitegemea katika nchi ni *Airport*, Bandari, Masuala ya *Infrastructure* na suala la Ulinzi na

Usalama na vyote Zanzibar tunavyo. Tunachotakiwa kukifanya ni kujenga mambo mazuri kujenga *infrastructure* nzuri katika *Industrial Park* katika barabara umeme uwepo wa kutosha kama nilivyosema kwenye muelekeo huu tunaitaji umeme mbadala na umeme vizuri tuwe nayo yote miwili umeme wa gesi tuwe nao na umeme wa jua tuwe nao siku ikitozea huku kumefeli huku kunafanyakazi na umeme wa Tanzania Bara uwepo.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tukiwa na umeme wa aina tatu unatutosha na nchi itakuwa *stability* yake itakuwa nzuri na hata ma-*investors* watavutiwa. Kwa sababu *investment* yoyote iliyokuwa kubwa na hususan kwenye viwanda kama umeme utakuwa bei kubwa watu hawatokuja kuekeza, vitu ambavyo vinawavutia ma-*investors* wote duniani ni masuala ambayo ya umeme kuwa bei chini *infrastructure* barabara ziwe nzuri, maji yawepo *on site* na umeme uwepo kwenye *on site* pamoja na vipaumbele vya ma-*investors* vinavyowavutia kwenye masuala ya kodi na masuala mengineyo katika nchi.

Tunavyokwenda kwa serikali hii tunayaona ndani ya siku mia moja labda na mbili ni mambo mazuri na tutafanikiwa na naamini tukianza kupata gesi, mafuta Bandari ikimaliza *Airport* ya Zanzibar ikimaliza na masuala mengime muhimu yakimaliza basi nchi hii Zanzibar itakuwa haishikiki na Mhe. Waziri naamini kwenye mwaka 2324 kama tutakuwa hai hii bajeti unaweza kukaja kuibalisha na ikafika kwenye trilioni tatu na milioni mia mbili. Hii naamini ni *target* ni makisio tu lakini tutakapokwenda vizuri mambo yanaweza yakabadilika ndani ya mwaka mmoja na nusu mpaka miwili, naamini tutafika pazuri na hatutotegemea tena ruzuku na kama ruzuku zitakuja itakuwa zinakuja kwa hisani na tutazipokea.Lakini kwenye bajeti yetu tutazifuta na zitakuwa hazimo na hatutoonesha kwamba tunagemea mtu na uwezo huo tunao na Mhe. Waziri wa Fedha nina imani sana na wewe. Lakini pia nakuomba sana tufanye kazi kama tulivyoanza bila ya kumuonea mtu huruma, tufanye kazi tuweke kipa umbele kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, suala la viwanda twende kwenye kodi Mhe. Rais aliahidi kwamba kodi ataishusha na naamini ataishusha kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Vitu ambavyo tunavihitaji katika nchi yetu sasa hivi tuna hoteli mia nne na kitu ndani ya Zanzibar lakini kodi tukiishusha hoteli zitafika hata elfu moja na mia mbili. Sasa hivi kuna maeneo zaidi ya mia sita ndani ya maeneo ya bahari hayajakuwa *invested* hayajajengwa mahoteli, lakini tutakaposhusha kodi viwanda vitakuja kujengwa vingi, mahoteli mengi, nyumba zitajengwa nyingi za biashara na masuala mengine. Kwa nini nikasema hivyo, unapoweka ushuru mkubwa, unapoweka kodi kubwa katika nchi wafanyabishara watakuja mia mbili. Lakini utapoweka ushuru mdogo ukaupunguza wafanyabiashara watakuja mia nane, matokeo yake nini ajira zitazidi kodi kwa serikali itazidi lakini pia kitakachokuwa *invested* kitakachowekezwa katika nchi serikali na nchi inapata thamani kubwa kwenye masuala ya uchumi.

Mfano leo tukijenga kiwanda kitakachoajiri watu elfu moja mia tano au tukijenga hoteli yenye vyumba elfu maana yake hata kama nchi rasilimali zake na *security* ya nchi inazidi kupanda thamani kwa sababu ya vitu ambavyo viliokuwepo. Ningemshauri sana Waziri wa Utalii ni vizuri mkawatafutia maeneo wenye mahoteli majina makubwa mfano *Sheraton, Hilton, Hayyat Regency, Tajmahal* na hoteli nyingine ambazo kubwa duniani, kila zikiwepo ndani ya nchi maana yake kwamba wageni pia waliokuwa wana uwezo mkubwa wanaona kwamba nchi hii ina *security* na nchi hii ni kubwa.

Mhe. Naibu Spika, majina tuliyokuwa tunayo sasa hivi ndani ya nchi yetu ambayo ni maarufu duniani hayazidi zaidi ya matano *Park Hayyat, Serena, Melia* na *The Residence* haya ndio majina ambayo duniani yanafahamika na ukienda katika dunia hoteli hizi bado sio kubwa. *Park Hayyat* ni *four star* katika dunia na wala sio *Five Star*. *The Recidence* ni hoteli kubwa sasa ukiangalia majina makubwa katika hoteli Zanzibar bado ni changamoto. Tafuteni wenye majina makubwa waje wa-*investment* Zanzibar ili tuone sasa Zanzibar infaidika vipi kwa majina kwa sababu jina pia linauza nchi.

Vile vile katika watu ambao tunawapa ubalozi tutafute watu wenye kufahamika si vibaya mkamualika Cristiano Ronaldo, Mesi wachezaji Mohamed Sala waje kutembea Zanzibar serikali na wizara mkawahudumia mahoteli vyumba na masuala mengine. Wakija wale Cristiano Ranaldo ana-*followers* milioni mia sita katika *Face book* na *Instagram* na *Twiteer* aki-*post* tu kaja Zanzibar maana yake utangazaji tosha kuliko *CNN*, *CNN* inawezekana inatizamwa na watu milioni kumi. Lakini Christiano akiposti picha moja watu milioni 400 wanangalia kwa siku, sasa kuna vitu mupate ushawishi wa kuwatafuta watu maarufu muwalike serikali muwaharime na matajiri wengine wetajitolea wenyewe kuja bila ya kutaka kufadhiliwa ni vyema mkatangaza sasa mnawaalika watu maarufu. Leo tumeona mnawapa watu ubalozi katika nchi hajulikani hata na watu milioni 2 ubalozi huo unafanya nini katika Zanzibar.

Zanzibar ni nchi ambayo inafahamika duniani ingieni kwenye nchi ambazo Zanzibar bado haijatambulika nendeni kafanye matangazo kwenye nchi ambazo Zanzibar haijui, juzi nimeona Bulgaria *aircraft* zipo tatu ni vizuri, Bulgaria ulikuwa ukienda ukawauliza Bulgaria kafanye *research* asilimia 90 wabulgaria hawaijui Zanzibar. Ukienda baadhi ya nchi Slovakia ukienda Macedonia Zanzibar hawaijui vizuri. Sasa kuna nchi wananchi matajiri Brunei, Singapore na nchi nyengine, Mhe. Waziri wa Utalii nakuombeni sana mumuombe Mhe.Rais mkasafiri mkatangaze nchi katika nchi ambazo Zanzibar bado haijulikani kwa nchi ambazo zinajulikana fanyeni kazi na mabalozi, fanyeni kazi na wafanyabiashara wakutangazieni nchi.

Zanzibar itafika wakati tutaingiza hiyo *airport* ni ndogo hiyo *airport* tutakayoifungua sasa hivi baada ya mwaka mmoja na nusu itakuwa watu wanakaa mpaka nje foleni,. Ni vyema sasa tunafungua *terminal III* lakini *terminal IV* tuanze kuandaa mikakati ya kuweza kujenga *terminal IV* Zanzibar, *Airport* ile ni ndogo sana wageni milioni 1.6 ni ndogo. Mhe. Naibu Spika, tutafika sana na tutafika kwa sababu tutasaidia mimi mawaziri wote nawatakia kila la kheri nawapenda na nataka tuwasaidie lakini nitakachowaomba kwenye kila waziri aliyeguswa katika masuala haya katika kitabu hichi ni vyema akasimamia na haya mambo yakaweza basi tutafika pazuri kweli na itafika wakati hakuna mwakilishi atakaeinuka ndani kumsema mtu.

Wa kwanza mimi leo kwenye huu muelekeo tu sijui hata nichangie wapi kwa sababu mambo mazuri yote yanavutia humu ndani, ndio maana nikasema naomba dua tufanikiwe kama tunavyotaka na kwa mwenendo uliokuwepo Mhe. Rais alioanza nao na nguvu zake na Mhe. Makamu wa Kwanza na wa Pili na Mawaziri hivi tunavyokwenda basi nina imani kubwa Zanzibar ndani ya miaka 5 maslahi ya Wazanzibari yatabadilika maslahi ya waheshimiwa yatabadilika.

Lakini nishukuru jambo la mwisho Mhe. Rais kwa ziara zake anazofanya kutembelea viongozi wastaafu na walikuweko nchini namshukuru na nampongeza sana naona anatembelea viongozi

lakini apange sasa kuanza kutusalimia na sisi wadogo majumbani kwetu akipenda aje atusalimie siku moja moja tutafurahi sana.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono mwenendo wa bajeti hii na nampongeza sana kwa asilimia mia moja ahsante sana.

**Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii niweze kuchangia hutoba ya muelekeo wa Hali ya Uchumi Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022/2023/2024. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwepo siku ya leo kuwa wazima wa afya lakini pili nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji wake lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kutuletea Hotuba ya Muelekeo ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo ya Bajeti ya mwaka 2020/2021.

Mhe. Naibu Spika,mimi nije moja kwa moja katika kitabu cha hotuba katika ukurasa wa 4 kwenye mfumko wa bei, Mhe. Naibu Spika hotuba ya Mhe. Waziri inaonesha kwa mwaka 2020 Julai Desemba kasi ya mfuko wa bei ya bidhaa na huduma imeshuka wastani wa asilimia 1.9 kutoka mbili 2.6 kwa kipindi kama hicho cha 2019/2020. Mhe. Naibu Spika, pamoja na hali hiyo kwa 2020 lakini kwa mwaka 2021 kuelekea 2022 hali ya mfuko wa bei na vyakula na bidhaa za huduma inaonekana kupanda hasa vyakula muhimu kama mchele, unga na sukari.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja atufafanulie huko tunakoelekea 2020/2021/2022 hali itakuwaje na serikali inajipanga vipi kudhibiti mfuko wa bei hasa kwa bidhaa za chakula ambazo ndio zinawaumiza wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nije katika ukurasa wa 12 katika deni la taifa Mhe. Naibu Spika inaoneka deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 9 ukilimganisha na mwaka 2019/2020. Waziri katueleza bado hali ya deni letu ni hilimivu lakini kama waziri alivyosema bado kuna mikopo inayoendelea kuchukuliwa katika miradi mikubwa. Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu kama nchi tuendelee na juhudi za kukusanya au kuimarisha mapato ya ndani na kudhibiti uvujaji wa mapato. Baadhi ya miradi yetu tunaweza kutekeleza kwa sehemu kubwa ya fedha zetu wenyewe na kupunguza utegemezi wa mikopo.

Mhe. Naibu Spika, nafahamu sana na sote ni mashuhuda na tunafahamu kasi ya serikali yetu ya awamu ya nane ya udhibiti wa mapato namuomba sana Mhe. Waziri tuzidi kuendelea na kasi hii hiyo lakini pia tumeona kwamba kuna taasisi zinaingiza fedha nyingi mfano Bandari lakini muda mwingi udhibiti wa fedha katika maeneo hayo yalikuwa sio mazuri. Nina imani katika hili muda mrefu wa udhibiti huo wa fedha ulikuwa sio nzuri lakini kwa sasa mapato yetu ya ndani yaweze kutumika vizuri na tuweze kufadhili wenyewe miradi yetu mikubwa ya ndani.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 21 katika vipa umbele vya kitaifa 2020/2022 katika vipa umbele vya kitaifa 2020/2022/2023/2024. Mhe. Naibu Spika, kwanza niunge

mkono vipa umbele vya kitaifa kama alivyoeleza Mhe. Waziri lakini Mhe. Naibu Spika, naomba sana nataka niseme kwenye kipa umbele cha kwanza cha kuimarisha miundo mbinu ambayo kuna ujenzi wa bandari ya Mwangapwani, ujenzi wa uwanja wa Ndege Pemba pamoja na barabara yenye kilomita 135 na kadhalika.

Mhe Naibu Spika, utaona miradi hii ni ya fedha nyingi ambazo nyengine serikali itatoa mfukoni na nyengine tutapata mkopo au msaada kwa washirika wa maendeleo. Sasa Mhe. Naibu Spika hoja yangu na nimuombe sana Mhe. Waziri miradi hii ni mingi ya ujenzi na inapomalizika inaachwa tu hakuna fedha zinazotengwa kwa makusudi kuhudumia miradi hiyo. Mhe. Naibu Spika, nakumbuka Baraza lako hili liliwahi kutoa ripoti ya kamati teule ya majengo ya skuli za serikali 19 ambazo zilipata matatizo ya kuvuja. Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kama lilivyo jina lake Fedha na Mipango katika mipango yao na nimuombe sana Mhe. Waziri apitie ile ripoti kwa kiasi gani katika mipango yake anaweza kuziweka fedha maalum kwa ajili ya ukarabati wa skuli zile.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti ile moja ya mapendekezo ya ripoti ile ni serikali kuwa na bajeti maalum ya matengenezo ya majengo yake ili kupunguza uchakavu na maharibiko yanayojitokeza. Nimuombe sana Mhe. Waziri skuli 19 ni nyingi na skuli zile hivi sasa wakati wa jua walimu na wanafunzi au maeneo husika ndio skuli zile zinawapa tija. Lakini keshokutwa hapa mwezi wa tatu tukijaaliwa ikianza masika zile skuli kama chungio hazifai na walimu na wanafunzi wanakosa sehemu nzuri ya kujifunzia. Nadhani katika hotuba yako Mhe. Waziri moja katika kusisitiza kwako ni suala la elimu na waheshimiwa wengi walikuwa wakichangia hapa katika vipindi vilivyopita kuhusiana kama jana walizungumza suala zima kuhusiana kwamba watoto hawafanyi vizuri mitihani, kumbe pia inawezekana yale mazingira ya kujifunzia kama hayako rafiki basi nina imani watoto wetu hawatoweza kufanya mitihani yao vizuri. Mhe. Naibu Spika, nikuombe sana miradi hii ya ujenzi ya miundo mbinu inapomalizika baada ua muda basi iwekewe fedha za matunzo yaani *maintenance*.

Mhe. Naibu Spika, tunaona hapa katika kipindi cha mvua barabara nyingi zinaharibika na tunalazimika kutumia gharama kubwa za kuzitengeneza, ingawa najua kuna mfuko wa barabara ambao upo lakini niombe sana katika maeneo haya niliyoyazungumza, basi iwekwe mifuko ya bajeti maalum ya matunzo ya ujenzi huo.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kipengele cha pili cha kuimarisha sekta kuu za uchumi. Mhe. Waziri nimuombe na nataka tupatie ufafanuzi katika mambo haya mawili kwanza kuimarisha mfumo wa kodi kwa kuweka chombo kimoja cha kodi ambacho serikali imeweka mpango gani sasa baadhi ya kodi zinazokusanywa na *TRA* kama zipo lakini pia ziweze kukusanywa na *ZRB*. Mhe. Naibu Spika, pia kuwepo kwa mfumo wa *one stop centre* ya kodi ni jambo zuri na litasaidia utitiri wa kodi na kuwafanya wananchi waone kulipa kodi kwao sio adhabu.

Mhe. Naibu Spika, la pili kuanzishwa kwa mfumo wa Bima ya Afya Mhe. Waziri jambo hili nimelifurahia na nina imani waheshimiwa wengi wamelifuriahia kwa kuona serikali ipo *serious* maana Mhe. Rais alilisema kwenye hutuba yake ya ufumbuzi wa Baraza la

Wawakilishi hapa na naona katika mpango huu serikali imeliweka katika vipao mbele vyake Mheshimiwa niwapongeze sana na tunawashukuru kwa hilo. Mhe. Naibu Spika, bima ya afya sio dhambi kuwepo katika mfumo wetu wa afya. Nakumbuka mwaka 2016 tulipitisha hapa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na wadau ambao tuliowalika katika kupitia ile miswada walipendekeza sana wakati umefika sasa Zanzibar tuelekee kwenye mfumo wa Bima ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, nina imani mfumo wa bima ya afya kwa wananchi wetu watauridhia na watakuwa wanafuraha na tuna furaha sana kuona kwamba awamu ya nane imeliona na imelichukua na nawapongeza sana. Mhe. Naibu Spika, katika kipaumbale cha tano ukurasa 22 kuimarisha utawala bora kuna suala la kukabiliana na athari za mazingira na mabadiko ya tabia nchi. Mhe. Naibu Spika, hapa sijaona mikakati thabiti ya serikali katika suala hili hivyo nataka nimuombe Mhe. Waziri sijajua hatua gani za udhibiti au ongezeko la kina cha maji ya bahari ya nchi yetu kwa sababu ni nchi ya visiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mahoteli mengi yaliyokuwepo katika maeneo yetu haya kwamba tayari kuna hizi *swimming pool* ambazo wanamwaga maji yao baharini kwa hivyo inaonekena inawezekana ikaleta athari katika shughuli zetu za uzalishaji. Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri aangalie udhibiti wa bahari na uchafuzi wa mazingira ya bahari kutoka mahoteli na viwanda na utupaji wa takataka za plastik. Tunaelekea kwenye uzalishaji wa uchumi wa bahari lakini kama bahari zenyewe hazitakuwa safi na salama katika mazingira yake basi changamoto zinaweza zikajitokeza katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba hili la mazingira ya bahari yetu serikali iweke katika mikakati madhubuti ili uchumi wa bluu uweze kufanikiwa. Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri serikali ijipange katika kutoa mafunzo kwa wale wakulima wa mwani lakini na wavuvi ili waendane na kasi ya huo uchumi wa bluu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache nakushkuru sana kunipatia nafasi hii na namuomba Mwenyezi Mungu amjalie Rais wetu wa Zanzibar lakini pia na Mhe. Waziri ambae amemteua ili kutekeleza majukumu haya yote katika hotuba hii ya muelekeo lakini pia na mawaziri wote ambao wataguswa katika maeneo haya, waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na tunawaahidi kama wawakilishi tutakuwa nao pamoja na waweze kutusaidia katika maeneo ambayo tunayaongoza ikiwa majimbo kwa sababu ndiko kwenye changamoto nyingi zinazowakabili wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniona kunipa nafasi hii adhimu lakini awali ya yote napenda kumshkuru Mwenyezi Mungu muumba mbigu na ardhi kwa kutupa uzima na uhai na kuweza kushiriki katika harakati hizi za maendeleo ya nchi yetu. Lakini kwa kipekee kabisa nachukua fursa hii Mhe. Naibu Spika, kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuonesha dhamira nia kwa maneno na vitendo kabisa kwamba analenga kuleta maendeleo ya Zanzibar kwa kiwango cha juu, tunoamba tumpongeze sana

Mhe. Rais na Mwenyezi Mungu sana amuongoze sana katika azma yake hiyo ili aweze kutufisha katika kilele cha mafanikio makubwa kupitia uchumi endelevu nchini Zanzibar.

Lakini vile vile kwa kipekee sana naomba kuchukua fursa hii adhim pia kumpongeza Mhe. Rais kwa kutuchagulia Waziri makini ambae ana mnasaba na taaluma yake katika sekta hii katika Wizara hii, lakini vile vile ndugu Jamal Kassim Ali kwa kutuletea hotuba ya hali ya uchimi mpango wa maendeleo na bajeti 2021/2022/2023/2024 ya kisayansi na yenye nia ya dhati kila mjumbe anakiri hutuba hii itaweza kutuvusha pale ambapo Zanzibar tunataka kuelekea.

Nampongeza sana Mhe. Waziri na nakuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kukuongoza ili uweze kushirikiana nasi na kukupa mashirikiano ya dhati kuweza kuleta maendeleo katika visiwa vyetu Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mimi nitajikita katika maeneo machache kutoa mchango wangu katika hotuba hii, hotuba ambayo imeonesha mambo mazuri mengi katika hayo na mimi nitachangia machache lakini zaidi nataka nizungumzie katika suala zima la uchumi wa bluu kupitia katika zao la mwani, ufugaji wa samaki, lakini nitazungumzia suala zima la mambo ya kale sambamba na suala la utalii kwa wote.

Mhe. Naibu Spika, zao la mwani ni moja katika vyanzo vipya au endelevu ambavyo vinaweza vikatuletea maendeleo ya hali ya juu kabisa katika visiwa vya Zanzibar. Zao hili kwa sasa linahitaji kupewa msukumo mkubwa na linahitaji kupewa nyenzo kubwa.

Ieleweke Mhe. Naibu Spika, kwamba hivi sasa Zanzibar ni nchi ya tatu duniani kuzalisha zao la mwani, sifa hii adhimu na kubwa iende sambamba na mnasaba na mukhtadha mzima wa kuwaangalia wakulima wanaozalisha zao hili la mwani kwa jicho kubwa na jicho la pekee. Haiwezekani kabisa katika mazingira magumu ambayo wanazalisha zao la mwani katika hali ngumu kidogo, lakini wameweza kutufikisha Zanzibar kuwa katika nchi ya tatu duniani kuzalisha zao hili la mwani na ni mwani ambao una sifa za kipekee. Vile vile Zanzibar hii ina sifa ya kwamba kuna uwezekano mkubwa kuwa kunazalishwa aina tofauti za mwani.

Kwa hivyo, kwa kipekee kabisa naiomba sana na ninaishauri wizara husika, kama hotuba ilivyokiona kipengele hiki, basi itowe umuhimu mkubwa katika uzalishaji wa zao la mwani, ikae na wakulima wanaozalisha zao la mwani sambamba na makampuni ambayo yananunua zao hili la mwani. Kuna uwezekano mkubwa kwamba Makampuni yanayonunua zao hili la mwani, kwa kiasi fulani hawawatendei haki wakulima wa zao hili la mwani.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali na wizara husika iandae kikao maalum ambacho kitawahusisha wadau wote wanaozalisha zao la mwani na Makampuni ya mwani, ili kulizungumzia kwa pamoja ni tatizo gani linalowakabili wazalishaji wa zao la mwani na kwa kiasi gani wanaweza kupewa moyo wazalishaji wa zao la mwani kuweza kulizalisha na ifike hatua kwamba zao la mwani wazalishaji wake wapate kunufaika kama wanavyonufaika katika zao la karafuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kipengele chengine ambacho naomba kukichangia ni suala la ufugaji wa samaki. Mhe. Naibu Spika, naipongeza serikali kwa kuja na wazo hili katika vipaumbele vya uchumi, ufugaji wa samaki ni ukombozi wa uchumi wa wananchi wa Zanzibar. Ufugaji huu wa

samaki utaweza kuwakomboa wananchi mbali mbali katika kujikwamua na tatizo la ajira, na ufugaji wa samaki una faida lukuki, na tuna maeneo ya kutosha katika suala zima la kufuga samaki katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Kwa hivyo, na hapa pia naishauri serikali iandae utaratibu maalum ambao utakuwa unatoa taaluma ya ufugaji wa samaki kwa wananchi, ili kila mwananchi taaluma hii aipate ibakie yeye mwenyewe tu kwa *interest* yake anataka kufuga au hataki kufuga, lakini elimu ya taaluma ya ufugaji wa samaki itapendeza sana kama kila mwananchi atakuwa nayo, kwa sababu tija na fanaka yake ni kubwa na inasemekana kwamba hata vile vidimbwi vidogo vya maji ya mvua unaweza ukafugia samaki, lakini ni lazima upewe taaluma hiyo. Kwa hivyo, naiomba sana wizara husika, hili ni eneo jengine ambalo serikali imeliona linaweza likawakomboa wananchi katika suala la ukosefu wa ajira.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni eneo la utalii kwa wote. Utalii ni uti wa mgongo wa uchumi wetu hivi sasa. Naipongeza wizara kwa kuweka kipa umbele hiki, lakini katika dhana ya utalii kwa wote kuna mambo naomba kushauri, jambo moja la msingi sana wananchi lazima wafahamu kwamba Zanzibar ni nzuri na Zanzibar tuna historia ya aina ya pekee, historia yetu imefungamana katika mataifa tofauti duniani, maeneo yetu ya kihistoria ni mazuri. Kwa hivyo, wananchi washajihike kwanza kuyatembelea maeneo yetu ya kihistoria, waweze kuyatembelea kwa hamu na shauku kubwa. Wakifanya hivyo basi watakuwa wanachangia pato la uchumi wa Zanzibar kwa asilimia kubwa.

Kwa hivyo, naiomba sana wizara husika taaluma hii ya utalii kwa wote iweze kusambazwa kwa hali ya juu kabisa, ili wananchi wawe na uzalendo wa kuipenda Zanzibar, waendelee kuipenda Zanzibar, waendelee kuvipenda vivutio ambavyo vinapatikana katika nchi yetu ambavyo havipatikani duni kote.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tuna pango moja Jambiani linaitwa *"Kumbi Café"*, pango hili lina historia pana ambayo kwa Afrika Mashariki na Kati nzima hakuna. Kwa hivyo, tunawaomba wananchi watembelee maeneo kama hayo, ili waweze kuona fahari na haiba ya nchi ya Zanzibar ilivyo.

Vile vile naishauri sana Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, katika dhana hii ya utalii kwa wote tujipambanue sasa. Tujipambanue sasa kuwa na aina ya utalii kwa sababu kisiwa chetu ni kidogo, sio vyema kuruhusu kwamba kila mawimbi, makundi sisi tuchaguwe aina fulani ya utalii ambao utakuwa na tija sana katika visiwa vyetu. Moja kati ya aina hizo ni watalii wenye mahitaji maalum, katika eneo hili bado hatujalifanyia kazi vya kutosha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, duniani kuna utalii huu wa watalii wenye mahitaji maalum, ambao *mostly* watalii hawa wanakuwa ni watalii wenye fedha nyingi na wanahitaji kutembelea maeneo tofauti. Hebu tunaomba eneo hili tuliangalie kwa kina sana, tujiandae vizuri kwa ajili ya kuandaa vifaa maalum ambavyo vitakuwa vinawapokea watalii hawa na kuwasambaza katika maeneo yetu tofauti ya kihistoria. Kwa hivyo, suala hili naomba sana lipewe maana litakuwa lina mchango mkubwa sana kuingiza pato la fedha za nchi za kigeni katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine katika mukhtadha huo huo wa utalii kwa wote, tuna utalii unaitwa *underwater archaeology* ni utalii unaopatikana chini ya bahari, bado eneo hili

hatujalifanyia kazi. Utalii huu unawahusisha watalii ambao wanakuja kutembelea chini ya bahari kuangalia *nature* ya maumbile na mambo tofauti ya kihistoria yaliyopita katika zama na zama na dahari ya nyuma. Zanzibar tuna utajiri mkubwa sana wa utalii ambao uko chini ya bahari, Zanzibar tuna meli nyingi sana zimezama ndani ya bahari watu wanataka kuziona, Zanzibar tuna matumbawe ya asili yenye upekee ambayo hayapatikani duniani kote.

Kwa hivyo, utalii huu ili uendelezwe Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale inahitaji kupewa mashiko, inahitaji kupewa nguvu. Kuna kitengo pale cha *underwater archaeology*, lakini kitengo hiki hakina wataalamu wa kutosha. Kwa hivyo, naiomba serikali na naishauri kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia kama kuna uwezekano katika vipaumbele vya taaluma basi kipa umbele cha taaluma ya *underwater archaeology* tukizingatia kwamba tunaelekea katika uchumi huu wa buluu, basi kipa umbele hiki kiwekwe. Wanafunzi waende wakasomee masuala haya ya *underwater archaeology* ili kuweza kuibua mambo tofauti ambayo yamo chini ya bahari, sambamba na kufanya tafiti mbali mbali ambazo zitatupelekea utalii wetu kwa jumla uweze kukua kwa kiwango cha juu.

Kwa hivyo, nashauri sana kwamba katika maeneo tofauti duniani, eneo la mambo ya kale linapewa thamani kubwa kama tunavyolipa thamani Zanzibar. Nashauri tuliendeleze eneo hili la Sekta ya Mambo ya Kale na kwa sababu watalii wengi wanapokuja katika nchi zetu kutembelea hamu zao kubwa ni kuona historia ya nchi, katika mambo ambayo wanakuja kuangalia nchini kwetu ni historia ya nchi. Katika historia ya nchi wanaangalia masuala hayo ya mambo ya kale na mambo mengine ya maumbile ya nchi.

Kwa hivyo, tutakapozidi kutilia mkazo suala hili, tutakapoyakarabati magofu yetu ya kale ambayo mengi yanaonekana kuwa katika hali dhaifu kidogo, ndipo tunapokuza na kuimarisha utalii wa nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hivyo, naishauri sana wizara kutilia maanani sana na zaidi katika kipengele hiki cha suala hili la mambo ya kale.

Mhe. Mwenyekiti, kipengele chengine ambacho nataka kuzungumzia ni ajira kwa vijana. Naiomba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, dada yangu Mhe. Tabia Maulid Mwita pale mweledi, mchapakazi na mahiri namuomba sana akiangalie kipengele hiki, ni kwamba kumekuwa kunatolewa mafunzo ya ujasiriamali mara nyingi katika sekta tofauti, lakini nadhani mafunzo haya ya ujasiriamali bado hayajawafaidisha vijana kuwapeleka kule ambako wanataka hasa kuelekea. Ni aina gani ya ujasiriamali ambayo tunaihitaji kwa vijana wetu, ni aina gani ya miradi hasa tunaihitaji kwa vijana wetu.

Kwa hivyo, tunaomba sana ufanyike upembuzi yakinifu na utafiti wa kutosha kabisa, ili kujua kwamba vijana wetu tunahitaji kuwapa ujasiriamali wa aina gani ambao utawakomboa katika maisha yao. Tumejaribu mara nyingi lakini hakukua na mafanikio kwa kiasi fulani. Lakini naomba kwa mfano mmoja kama vijana wataelekezwa katika ujasiriamali wa ufugaji wa samaki, Baraza lile la vijana likaandaliwa mradi maalum wa ufugaji samaki, basi nina imani kubwa kwamba kutakuwa na tija ya mafanikio ya hali ya juu sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki kueleza mengi sana, kwa sababu mambo mengi yameshaelezwa katika hotuba hii yote ni mazuri na yanalenga kuinua nchi yetu kwa maendeleo ya hali ya juu sana. Kwa hivyo, nimeona niyaeleze haya machache. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa

kunipa fursa hii. Mwenyezi Mungu ibariki Tanzania, Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Nimepata taarifa kwamba Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed tayari alishachangia. Sasa naomba nimpe nafasi Mhe. Haji Shaaban Waziri, atafuata Mhe. Ali Suleiman Ameir.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na siha nzuri, pili nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kwa kumshukuru Rais wetu wa Zanzibar, ukiangalia hiki kitabu namna kilivyotungwa basi utakubali kwamba kweli hawa ambao amewateuwa hakubahatisha, niwapongeze sana kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya hiki kitabu kuna maelezo mazuri yanaridhisha kiasi cha kwamba unapata matumaini mazuri, ila na mimi nataka kuchangia kwa kutoa indhari kwa baadhi ya maeneo. Nataka nianze eneo ambalo linauzungumzia ukulima juu ya umwagiliaji. Hapa nataka kuzungumzia juu ya miradi ambayo tunaifanya ya umwagiliaji, wakandarasi ambao wanatufanyia hiyo miradi pamoja na mikataba ambayo tunakubaliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, nataka kulisema hili lengo letu hapa linachoonesha wananchi wetu kuwa na manufaa juu ya miradi ambayo tunaifanya, sasa tusipokua makini tutakuwa tumefanya miradi lakini haikuleta manufaa.

Mfano, tunaumwagiliaji sasa hivi kwenye Bonde la Koani kumetengenezwa pale, lakini ukienda kuangalia kilichotengenezwa hakina manufaa, na wananchi wanalia wanasema ni kheri ingebaki vile vile. Sasa hapa kinachoonekana kwamba wale wakandarasi ambao wamefanya ile shughuli hawakuwa makini, kwa hivyo sasa imetuletea shida na pesa zetu zimepotea nyingi. Sasa maana yangu ni kwamba lazima tunapokwenda kwenye mambo haya tuwe tunaangalia vizuri kwenye maeneo haya.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka niende, nalo tuliangalie hapa, tumezungumzia ujenzi wa masoko. Ni kweli sisi Zanzibar bado tuna matatizo ya masoko. Mimi kabla ya kuingia kwenye mambo ya siasa nilikua nikifanya biashara ndogo ndogo kule vijijini, tokea kule soko la Darajani lile la ndani tukaja nje, tukaja nje huku kunakouziwa kuku, tukaenda pale ambapo sasa hivi pana Benki Kuu, tukaja hapa Kibandamaiti na tukaenda huku. Lakini kila siku ni kuhamisha hamisha watu kiasi cha kwamba hatuwezi tukajenga soko lenye uhakika. Utaona hivi karibuni tu watu wamehamishwa Mombasa wakapelekwa Jumbi pale wamekwenda kutupwa tu, lakini sasa hivi tayari tunalizungumza soko la Jumbi, lakini tumelitengeneza katika mazingira yepi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ushauri wangu katika hali hii. Niliwahi kutembea nchi ya Burundi nimeona wenzetu wa Burundi pale wanawapa watu binafsi kujenga masoko, sasa huyu mtu yeye na serikali juu ya kulipana itakuwa kwao, lakini na yeye juu ya wafanyabiashara itakuwa juu yake. Kwa hivyo, tufikie mahali na sisi tuwape watu nafasi wajenge masoko, ili masoko yatu yawe yenye uhakika tusiwe tunawatupa tupa tu watu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili tunazungumzia kwenye ujenzi wa nyumba za makaazi. Mimi hapa nilikuwa nina mashaka kidogo, tunazungumzia nyumba za makaazi za nani, maana nina wasi wasi tusije tukarudi tulikotoka, tukawa tunajenga nyumba za makaazi lakini baadae tukawa tumegawa matabaka, kwamba wenye tabaka hili ndio wanaoweza kukaa nyumba hizi, na wenye tabaka hili wanaweza kukaa nyumba hizi.

Mfano mzuri uko kwenye nyumba ambazo zimejengwa Mbweni, baadhi ya wananchi wetu hawawezi wakaishi kwenye nyumba zile. Sasa je, na hizi tunazojenga tumelinganisha namna gani kwa wananchi wetu wote, ndio huo wasi wasi wangu ulipo hapo.

Kwa hivyo, kama tunakusudia kujenga nyumba za makaazi, basi tuwe tunajenga nyumba ambazo tunaweza tukamuweka mwananchi yeyote Mzanzibari na yeye afaidike na matunda hayo, ndio *target* yangu ilipo hapo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nazungumzia ujenzi wa vituo vya daladala, maana hili mimi naliunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia, kwa sababu sisi Zanzibar vituo vya daladala hatuna hata kimoja. Sisi watu ambao tunaishi vijijini kule ukweli tunapata shida tunapokuja mjini. Kituo chetu cha Mwembeladu pale, sijui kina miaka ishirini na ngapi au thelathini na ngapi, lakini hakuna huduma ya choo hadi leo. Mtu umekuja pale na mgonjwa wako unampeleka Mnazi Mmoja, unakuja naye pale akihitaji choo hapati.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tukaanzishiwa kituo chengine Welezo pale, kituo kiwe Welezo kituo kiwe Welezo hapana huduma ya choo si kituo cha daladala. Kwa hivyo, lazima tufikie mahali tunapozunguzia kituo cha daladala basi kiwe kituo cha daladala kweli na kiwe kinaweza kumsaidia mtu kwa hali yoyote, leo hapana hata huduma ya aina yoyote. Lakini hatimaye unakuja kuambiwa kwamba usichafue mazingira, hivi mtu yule anapokuwa na haja aende wapi na watu wengine wageni hapa mjini. Sisi tunaotoka vijijini hatuna nyumba huku mjini hatuna ndugu, ina maana tunakwenda *stand* tunajua hapo ndio pakumalizia harakati zetu. Kwa hivyo, nilikua naomba tufanye haya mambo yawe yanatizamika, yawe yana viwango na tusiwe tunazungumza tu kwa kufurahisha.

Kwa hivyo, mimi naomba kwamba kama tunaweza kufanya mambo hayo tunaweza tukafikia pahali pazuri zaidi.

Baada ya hapo mimi naunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia kwenye hili.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Haji Shaaban Waziri. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Ali Suleiman Ameir, ajitayarishe Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

**Mhe. Ali Suleiman Ameir:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hoja ambayo iliyokuwepo mezani, ambayo inahusu Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa muda wa Kati.

Mhe. Naibu Spika, pili nimshukuru Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango kwa kuweza kutuletea mpango huu. Hotuba hii ambayo ni nzuri ambayo ni muelekeo wa yale

ambayo tunategemea twende tukayafanye. Lakini nimshukuru Kamati ya Bajeti na wao kwa kuweza kuyaeleza yao yale machache ambayo wameyaona na yanayoweza kuisadia serikali na sisi Wajumbe katika kuchangia mpango huu.

Lakini kabla sijaanza kuchangia naomba Mhe. Naibu Spika, uniruhusu kunukuu maneno machache ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika hotuba yake ya tarehe 11/11/2020 ya ufunguzi wa Baraza hili naomba kunukuu.

“Mimi na nyinyi tumeshirikiana katika uchaguzi na kufanya kampeni, tumewasikia wananchi wetu na matarajio yao kwetu kote nilipopita mimi na bila ya shaka nyinyi mmekutana na kiu kubwa ya wananchi wetu ya kutaka kufanya maisha yao kuwa bora zaidi. Wametuchagua kwa sababu tumeahidi kutimiza mataraji hayo. Aidha, heshima itatokana na sisi kutimiza matarajio yao. Heshima yetu itatokana na sisi kutimiza ahadi zetu maana sio tu kwamba ahadi ni deni bali kutimiza ahadi ni kulinda heshima”.

Mhe. Naibu Spika, heshima ya wananchi wa Zanzibar lazima ilindwe kwa kuwaletea maendeleo. Ndio wanachokihitaji hawahitaji kitu chengine chochote.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwenye kuchangia hotuba hii hali ya uchumi wa Zanzibar niwaombe wezetu Wizara ya Fedha na Mipango katika kupanga mipango yetu tuangalie nyenzo ambazo zinatokana na ndani bila kuangalia nyenzo zile za kidunia sana. Tuangalie hali yetu ya biashara, tuangalie hali yetu ya utalii na tuangalie hali yetu ya usafirishaji mazao nje ya nchi. Vitu hivi vitatu vitatupekea hali ya uchumi tunayoitaka ndio ambayo tutakuwa tunaweza kuipeleka mbele. Lakini kwa kuangalia tu vigezo kutoka nje bila kuangalia vigezo vyetu vya ndani hatutoweza kufanikiwa kule ambako tunataka twende.

Lakini pili, mipango ya maendeleo basi tupange kwa yale ambayo yanatekelezeka lakini tupange kwa yale ambayo ni ya dhati tunaamua kwamba haya tunayapanga na tunaenda kuyatekeleza. Lakini tusipange yale ambayo tumeamua tu tuyapange japo yatakabakia kwa muda mia mine, mitano, sita, yamo kwenye makaratasi tutakuwa bado tunajidanganya sisi wenyewe. Mhe. Naibu Spika, nimuonbe Mhe. Waziri tuangalie kupanga kile ambacho kinaweza kutekelezeka.

Baada ya hapo moja kwa moja Mhe. Naibu Spika, niende katika vipaumbele vya taifa vya maendeleo. Sekta ya Uvuvi ni sekta muhimu inahitaji nguvu inahitaji kulindwa. Mhe. Naibu Spika, niwaombe serikali na wizara husika inayohusiana na Uchumi wa Buluu kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kwa lengo la kuweza kuwasaidia wananchi kuweza kujiajiri. Ili waweze kununua vyombo mbali mbali vitakavyowesha vyombo hivi kuvua raslimali hii ambayo ipo baharini. Raslimali hii ikivuliwa ipasavyo itaweza kutusaidia, bahari ndio mashamba yetu na mashamba yetu tunatakiwa tuyatumie ipasavyo, tunavyoweza ili yaweze kutuletea tija. Kuwapatia vyombo vya kisasa wavuvi hili ni kitu muhimu ili wavue kwa tija lazima wawe na vyombo vya kisasa, kuwapatia nyenzo za kifedha tuhakikishe kupitia vyanzo vyovyote vya ndani na nje kwamba lazima wavuvi wale wapate vyanzo vya fedha ili waweze kwenda kule mbele bila ya kuyapanga haya watakuwa hawawezi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, wamevuna raslimali wanaipeleka wapi, masoko ya kisasa masoko yenye tija ni kitu muhimu lazima liwepo ili uvuvi uweze kuwa na tija zaidi. Lakini viwanda ni kitu cha muhimu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye *issue* ya bandari, ndio mlango mkuu ambao unaweza kutupatia fedha hususan mapato ya ndani. Wakati umefika kwa Shirika la Bandari kuipa vyanzo mbali mbali vya kutendea kazi, niombe serikali ina azma ya kuendeleza bandari mbali mbali ya Mpigaduri, Mangapwani, Mkoani, na Wete lakini ni wakati sasa hivi hichi tulicho nacho tuweze kukipa nguvu zaidi tuweze kuwapatia vifaa vya kisasa ili viweze kufanya kazi ipasavyo.

Lakini Bandari ya Mkokotoni sikuiona kwenye vipaumbele bandari ile inatusaidia ni bandari ambayo tutapoweza kuihimili itakuwa yanashindwa yale magendo ambayo yanapatia katika bandari ile kupungua. Niombe tueke mkono kwenye Bandari ya Mkokotoni ili suala la biashara ya magendo iweze kuondoka. Lakini tuimarishe huduma za kisasa kwa ajili ya ushushaji na upakiaji wa mizigo ikiwemo makontena. Vifaa viwe vingi mfano *reach stacker, winch crane, truck, forklift, sprader,* ni vitu muhimu wafanye kazi lakini tuwape vyanzo vya kuweza kufanya kazi nikuombeni serikali mushiriane ili viweze kupatikana.

Lakini wapunguze idadi ya kushughulikia meli sasa hivi meli moja inashughulikiwa kwa siku 7 ambayo hii inaathari kwamba tayari mali ipo inataka kushuka Zanzibar lakini uwezo wa kushuka hakuna, meli zinabadili muelekeo na kwenda kushusha Mombasa na Dar es Salaam na wakati tuwapatie vifaa lakini ni wakati wa sasa hivi watendaji wetu waweze kuitumia rasilimali ya bandari ili kuweza ufanisi. Niwaombe kwa sasa wana uwezo wa kushusha kontena 80 hadi 40 kwa *shift* moja masaa manane basi tuende kwenye kontena 160 ili tufikie lengo tukiwa na uwezo wa meli Zanzibar zinakuja kwenye *choose* 540 mpaka 1,200 tukayaweza haya tutahudumia meli kwa muda wa siku 3 hadi 4 tutakuwa tumo sambamba katika Afrika Mashariki tunakweda sawa niwaombe tuweze kufanya hilo tuweze kufanikiwa.

Barabara ni kitu muhimu naomba kuuliza swali kwenye ukurasa wa 22 kuna barabara mliweka ya Wete-Chake Chake je lile tatizo sugu ambalo kwa miaka mitatu ya kibajeti limejitokeza la masharti ya *Saud Fund* na *BADEA* ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano walishindwa kukubaliana nayo yameondoka na kama yameondoka je, kwa sasa hivi nani ambaye atakuwa mfadhili wa barabara hii na mmesema mkataba tayari uko tayari kuingizwa naomba tupate ufafanuzi wa barabara hii ya Wete-Chake Chake je, bado tunaendelea na *BADEA* na *Saud Fund* au tuna mkataba mwengine ambao tutafanya.

Lakini tumekubaliana kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio kigezo cha mgawanyo wa rasilimali matumizi katika muundo kwamba tutajenga kilomita 197.6 za mtandao wa lami. Lakini nashangaa kwa mwaka huu tumeweka kilomita 22 peke yake, lakini kwa mwaka wa muda wakati tulimeweka kilomita 135 sawa sawa na kilomita 40 kutekeleza kwa mwaka husika. Hatuoni tunajidanganya kwamba tunajenga kilomita 22 wakati uwezo wetu na hali yetu ya kujenga kwa mujibu wa ilani inayotuongoza ni kilomita 40 au 45. Niombe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tusijidanganye Tume ya Mipango kile tunachoweza kukifanya kwa lengo la kuleta heshima kwa wananchi.

Nikuombeni kwamba tuongeze na barabara mbili barabara ya Tunguu - Jumbi yenye kilomita 9.3 hii ni barabara na ni ya kimkakati, niombe basi ili tufikie kwenye kilomita 40 kwa mwaka tuiongeze na barabara hii katika kipa umbele cha mwaka huu. Lakini tuiongeze barabara ya Fumba–Kisauni imekuwa ni dane dane miaka mingi nikuombeni serikali barabara hii tuendelee kuweza kuifanyia kazi, lakini halmashauri ziendelee kukusanya mapato ili tuwe kufanikisha.

Mhe. Naibu Spika, suala la karafuu jana Mhe.Waziri anajibu swali la msingi la Mhe. Mussa Foum Mussa alisema ni tatizo la msingi ambalo karafuu kwa sasa hivi zimepungua kununuliwa na kwenda nje kwa sababu Shirika linashindwa kununua kutokana na madeni mengi. Lakini kwenye hotuba yako kwenye ukurasa wa 5 umesema tatizo ni kutokuwa na bidhaa hii kutoka kwa wakulima lipi sahihi jibu la Mhe. Waziri anayeshughulika masuala ya biashara, jibu la Tume ya Mipango naomba tupate jibu kwa sababu nakisi ya biashara itaendelea tusipokuwa tuna-*export* ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, ajira kwa vijana, niiombe serikali ajira kwa vijana mradi huu utekelezwe kwa nia njema na utekelezwe kwa dhati na usibaki kwenye makaratasi. Bila ya vijana shupavu kuwezeshwa hatutakuwa na maendeleo hawa ni kundi ambalo kubwa lipo. Serikali imekuja na nia ya dhati mwaka wa kwanza bilioni 3, mwaka wa pili bilioni 2 basi niombe pesa hizi za ajira kwa vijana zitumike ipasavyo kwa mitaji ambayo inahitajika.

Lakini tuanzie kwa ile miradi ambayo itatuletea mafanikio kama vile ambavyo mimi ninachokumbuka kuna miradi mitatu kwenye meza ya Tume ya Mipango lakini haiwezi kutekeleza haitakiwi kutekelezwa, sijui sababu nini inatekelezwa miradi ambayo hata uchambuzi yakinifu hakuna. Mradi wa Machinjio ya Kuku, Mradi wa vingashio na Mradi wa Usarifu taka upo Tume ya Mipngo na ni agizo la Baraza la Mapinduzi itekelezeni miradi hii nikuombeni ni wakati sahihi wa kuitekeleza miradi ile kwa maslahi ya vijana.

Mhe. Naibu Spika, *program* za kuwajengea ujuzi *technical vocationary education training* ndio njia sahihi ya kuwaokoa vijana. Kwa sababu *self employment* na kuwaajiri serikalini ni vitu viwili viende sambamba nikuombeni muekeze kwenye program za wanagenzi *intership program, transfer of skills* na *recognition prior learning*.

Mhe. Naibu Spika, niweze kumalizia kwenye suala la viwanda tujiekeze kwenye viwanda, bila ya viwanda shupavu bila ya viwanda imara hatutoweza kufika kule ambapo tunatakiwa tufika. Niiombe serikali tuhakikishe tunaekeza kwenye viwanda kama tuna nia ya dhati ya kweli ya kuondoka hapa tulipo lazima tuende kwenye viwanda, bila ya viwanda hatutokwenda tusitegemee utalii na kukusanya kodi peke yake. Lazima na sisi tu-*export* kwenda nje, niombe Kiwanda cha Sukari narudia tena ni kiwanda cha mkakati kipewe meno ili kitusaidie. Zanzibar *milling coporation* muekezaji yule alindwe apewe meno ili aweze kutusaidia. Kiwanda cha Maziwa kilindwe ili kiweze kutusaidia na viwanda vyengine vya kimkakati ikiwemo kiwanda cha mwani kile cha Chamanangwe ambacho kinaendelea lakini na maendeleo.

Lakini kuna suala muhimu la Tume ya Mipango mmekuwa mnapanga miradi lakini baadae miradi ile mnajipa nyie wenyewe nyinyi mnapanga nyinyi mnatekeleza, nyinyi pangeni na simamieni utekelezaji ule Mradi wa Mkurabita ni wakati sahihi mradi huu au mkaupeleka Mamlaka ya Uwezeshaji maana yake Wizara ya Kazi na Uwezeshaji au mkaipeleka Wizara ya

Biashara na Viwanda. Nikuombeni mradi huu utekelezaji sahihi usiendelee kubaki Tume ya Mipango tufateni kule kwa wenzetu. Lakini Mfuko wa Miundombinu kuna tatizo kidogo ukurasa wa 9 Mheshimiwa mmekusanya mapato ya bilioni 13.2 lakini matumizi ni bilioni 10.2. Kuna pesa imebaki ya bilioni 3 ya ziada *surplus* iko wapi, mbona hamkutueleza na kama imetumika imetumika imetumika kwa nini wakati kuna miradi bado hamjaitekeleza. Lakini mlipanga bilioni 44 kwa makusanyo bilioni 44.2 haya yalikuwa ndio matumizi kulikuwa kuna milioni 500 *almost* tulikuwa tutumie kwa mambo mengine ni wakati sahihi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumalizia ni wakati sasa wa kufanya *need assessment* tunahitaji nini lakini tukishakujua tunachokihitaji twende tukaangalie *capacity assessment* uwezo wetu ni upi. Lakini baadae tukaangalie *performance assessment* huko tunakotaka tuweze kwenda.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumalizia kwa mwisho mapato ya ruzuku na mapato ya mikopo. Sura ya kibajeti, kwenye sura ya kibajeti tunategemea kukusanya mapato ya ruzuku na mikopo ya bilioni 332.5 lakini tunategemea kutumia kwenye ruzuku na mikopo bilioni 334.4 kuna upungufu wa bilioni 1.9 tunazitoa wapi nalo hili Mheshimiwa utakapokuja uweze kuja kutujibu lakini mwisho namalizia kuna pahala tunataka tukawekeze mradi unaoitwa *international convention center* Nyamanzi.

Nimetembea kidogo sijapata kuona *international convention center* zikawa nje ya Miji duniani kote *international convention center* ziko Mijini *top ten international convention center* ni wakati sahihi *international convervation center* muweze kuileta Mjini. Ushauri wangu ikiwa tunakwenda kwenye mradi wa kimkakati eneo la Bwawani ikiwa tunatafuta ushirikiano na muekezaji tuboreshe eneo lililokuwepo mbele kwa ajili ya kujenga *international convention center*. Jina sio Nyamanzi tuna muasisi wa nchi hii apewe stahiki yake na malengo yake ya kuikuza nchi hii Abeid Amani Karume *international convention center* isimame ikiwa Mijini na Mjini ndio alipoweza kuanzia.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana lakini kupanga ndio matumizi tuna tatizo kwenye *ZBS* tumesema asilimia 40 ya utekelezaji wa mradi ofisi na vifaa vya maabara umekamilikia lakini pesa hazijatumika. Mhe. Makamu alikwenda pale na Mhe. Waziri alikwenda pale alikuta ujenzi upo pesa haikutumika tuambiwe basi ile *three billion* iliyopangwa kutoka kwenye Mfuko wa Miundombinu kama haitakiwi tena kwenda kutumika kule basi tuelezwe ili tupange kwengine tuweze kuitumia.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa, mchangiaji anefuata sasa atakuwa ni Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma ajitaarishe Mhe. Harusi Said Suleiman uliwahi kuchangia ? Atafuata Mhe. Harusi Said Suleiman na baada hapo ajitayarishe Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis (*makofi)*

**Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi niungane na wenzangu kwa kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia uzima pumzi afya na hatimaye sasa hivi kujumuika katika majukumu yetu ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu pia kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa kasi na nguvu ambayo aliyokuwa anaianza kwenye utekelezaji wake wa majukumu. Lakini jengine nimpongeze kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii ya muelekeo wa hali ya uchumi wa mpango wa maendeleo kwenye bajeti yetu kwa miaka hii ambayo imetajwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kutoa michango yangu kwenye hotuba hii kwa kugusa maeneo mbali mbali ambayo nahisi yakitekelezwa vizuri yataweza kutusongesha vyema ili mambo yetu yaende kama vile ambavyo yamepangwa. Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa ujumla kwenye kesi nzima hii ya hotuba yetu na kama ilivyobeba dhamira yake ya hotuba ya muelekeo wa kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niongelee kesi nzima ya ongezeko la pato la taifa sambamba na hilo imechanganuliwa vizuri pato la taifa litaongezeka na kuanzia asilimia 5 mpaka asilimia asilimia 7. Mhe. Waziri mimi nimuombe tuzingatie na hali halisi ya pato la mtu mmoja mmoja ukuaji wa pato la taifa liende sambamba na ukuaji wa pato la mtu mmoja mmoja. Kwa sababu gani, tukiangalia hali halisi ya uchumi wetu huko nje tunaona bidhaa haswa zile za vyakula na bidhaa za ujenzi zimepanda kwa kiwango cha juu. Sasa ili twende sambamba na hili ongezeko la pato basi tuone na sisi tuna miundombinu mizuri ya kuweza kuinua hali za kiuchumi za wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kitu chengine ambacho nataka kuongezea ni kwenye uk. 5, tunaangalia *figure* iliyokuwepo kwenye mwenendo wa uingiaji wa utalii nchini. Tumeona tuna upungufu mkubwa wa watalii wetu na sababu pia tumezitaja ni nini. Mimi nataka niongelee kwenye upande mwengine kwa ufasaha zaidi na bahati njema Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale yupo na tunategemea kwenye *figure* yake ya bajeti ya 2020-2021 atakuja na maeneo yale ambayo ame *target* kama ni vipaumbele kwenye kukuza utalii wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe Wizara husika ikishirikiana na Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo ambayo ina-*deal* na utamaduni, niiombe hali halisi ya utalii wetu tunaona ni vipi watalii wetu wanaingia nchini lakini ni nini wana *participate* kwenye uchumi wetu, lakini tusije tukajisahau tukatoka nje ya mstari tukayaondoa yale maadili yetu ya kizanzibari na kufuata maadili yao.

Mhe. Naibu Spika, hili naomba niliseme kwa ushahidi ambao sasa hivi upo katika mitandao lakini tunaona hali halisi za mitaani, watalii wetu sasa wameanza kujitoa kwenye maeneo ya utalii na baada yake wanaingia mitaani na huko mitaani wako kinyume na utamaduni wetu wa mzanzibari lakini kinyume na utamaduni wetu wa mtanzania.

Mhe. Naibu Spika, hilo eneo nimeona niligusie kwa sababu wahanga wakubwa wa uporomokaji wa maadili ni sisi vijana. Ikitekelezwa vizuri ajenda hii na wakishirikiana wizara na sekta hizo ambazo nimezitaja naamini tutautangaza vizuri utalii wetu, lakini Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale aone namna nyengine kama alivyogusia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf aone namna nyengine ya kuutangaza utalii wetu. Tutafute Mabalozi ambao ni maarufu lakini tuwatafute mabalozi ambao wanaweza kutusaidia moja kwa moja kuutangaza utalii wetu ndani lakini na nje ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye Uk. 23, nigusie *issue* nzima ya muelekeo na sura ya nchi yetu. Nianze kugusia vipaumbele vya kitaifa katika mwaka 2021-2022. Naomba turudi kwenye *reference* ya mwaka 2020-2021 tuliweka vipaumbele vya maendeleo kwenye kipindi hicho vipaumbele 13 na kwa bahati njema utekelezaji wake nadhani tutaujadili na tutaona hatua gani ambazo tumefanikiwa na hatua gani ambazo tumefeli. Lakini kwenye vipaumbele vya hii 2021-2022 kuna vipaumbele 17 ambavyo vimeoneshwa kwenye kitabu hiki.

Mhe. Naibu Spika, kama Mjumbe wa Baraza wa Wawakilishi na wasimamizi wazuri wa serikali yetu na sera yetu ya Chama cha Mapinduzi. Mimi niishauri wizara irudi ikajifungie ikaangalie vipaumbele gani muhimu ambavyo tunaweza kuvitekeleza kwa muda huu na kwa ufanisi zaidi.

Nimeshtushwa na hii namba ambayo ipo hapa, vipaumbele 17 na vyote vya muhimu na tunavihitaji kwenye nchi yetu kwa maana hiyo kwa maoni yangu na ushauri wangu, serikali irudi Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango ikaangalie yale maeneo muhimu ambayo tutayatekeleza haswa ukizingatia uchumi wetu umeshuka kidogo kutokana na hali ya janga la dunia ambalo linatukabili.

Mhe. Naibu Spika, kwenye vipaumbele hivi naomba nianze kuvisemea baadhi yake kama kipa umbele Nam.5, kuna *issue* ya kuendelea na Hospitali mpya ya Rufaa ya Binguni.

Mhe. Naibu Spika, niiombe wizara, hii Hospitali ya Binguni ipo kwenye mkakati tangu Mwaka 2016 kama mnakumbuka kwenye Baraza hili na kwa bahati njema kila bajeti inapofika hapa tunaitengea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa jengo hili.

Mhe. Naibu Spika, mpaka hivi ninavyosema na kupitia kitabu hiki cha Mhe. Waziri, tunaona utekelezaji wake upo katika asilimia ndogo sana. Mpaka sasa kuna jengo moja tu la *emergence* ambalo limekamilika na tukiangalia kila mwaka hapa ukifika tunatenga fedha zaidi ya bilioni kwa ajili ya jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwaombe wizara hili jambo ni muhimu na dhamira ya serikali yetu ni kuzipeleka huduma za kijamii kwa wananchi wake na kila tukija hapa tukisema tunafanya na mwisho wa siku tukiwa hatufanyi imani yangu ni kwamba nafsi zetu zitakuja kutusuta kwa kile kitu ambacho tulidhamiria kwa ajili ya wananchi wetu. Kwa maana hiyo Mhe. Waziri kupitia katika Sekta hii ya Afya nimuombe kupitia Mhe. Waziri atakaekuja Mungu akitujaalia inawezekana ikawa sisi miongoni mwetu washirikiane tuone hili jambo angalau liwe linaleta sura na tukiweza kusomewa ripoti tuone limetekelezwa kwa asilimia ambayo inaridhisha.

Mhe. Spika jengine niombe kwenye kesi hii ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Binguni niseme tuwashirikishe wananchi wetu katika maeneo hayo ipasavyo. Nimeona mradi huu umepewa wazawa na kwa bahati njema kama ni wazawa maana yake ni kampuni yetu sisi ya kizalendo. Lakini masikitiko yangu niseme kwenye ujenzi wa hospitali hii kwa hii hatua ambayo imeanza, kuna baadhi ya ubadhirifu ambao unatokana na sisi wenyewe wazawa. Kwa mfano, kwenye ujenzi wa hayo majengo ambayo yaliyokuwepo kuna vifaa vya ujenzi ikiwemo saruji, mabati na vitu vyengine, tunaona kampuni ambazo zimekabidhiwa au zinazosimamia zimekuwa zikitoa vifaa hivyo kiholela.

Mhe. Naibu Spika, kama wenyewe wananchi wapo wakishirikishwa ipasavyo kwenye maeneo ya ulinzi. Mimi naamini kuna baadhi ya vitu vitasemwa lakini pesa ya serikali nayo itabaki katika mikono salama.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kuendeleza programu ya ajira kwa vijana. Hapa wajumbe wenzangu wengi wamegusia na mimi kama Mwakilishi wa vijana sina budi kugusia *program* hii kwa vile ni mwathirika mkubwa wa hili jambo.

Mhe. Naibu Spika, tumetoka kuona utekelezaji uliopita. Sitaki kufufua makaburi ambayo yamepita lakini tukubali kwamba tulikosea kuwatekeleza ajenda hii vijana wenzetu lakini kwa sasa hivi waziri na uongozi ambao upo naamini kwa vile wengi wao ni vijana na wanaguswa na haya matatizo ya vijana naamini watatekeleza vizuri. Ombi langu kwao, wakae na vijana wenyewe, wakaibue miradi ambayo wanahisi wataitekeleza kwa matakwa yao wenyewe ili kuzinusuru fedha za serikali zisiende kupotea. Lakini jengine wawatafutie wataalamu vijana, kwa sababu vijana wanaibua *idea* zao tofauti, lakini ukizingatia hawana utaalamu wa kutosha waende kukaa nao, wawaongoze kwenye maeneo ya kuandaa *proposal* ya miradi yao ili wanapokuja pale ofisini kwao waweze kuwa *push* kwa mara moja na kuondosha ule mlolongo na urasimu wa kwamba nenda rudi na baadae kupewa miradi ambayo haimo katika vichwa vyao.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu ambacho nataka nikiseme, serikali iliandaa *program* ya ajira kwa vijana kwa lengo zuri lakini fedha na miradi hiyo na vifaa ambavyo vimekwenda kwa walengwa sidhani kama wanavitumia ipasavyo. Kuna baadhi ya vijana wao wana *idea* nyengine lakini wameletewa kitu kingine. Kwa maana hapo *totally* hawatakua na hamu wa shauku ya kwenda kuweza kufanya lile jambo wamelikusudia. Kwenye mambo ya miradi mengine wizara ipo tutakuja kuelekezana namna ya kufanya, lakini kuna kipa umbele kingine namba nane ni kuendeleza viwanda vyengine vidogo vidogo vya usarifu wa mwani, chumvi na samaki.

Mhe. Naibu Spika, hapa niseme kwamba, katika dhamira njema ya kuendeleza maslahi ya nchi yetu, serikali yetu imeona kwamba igusie maeneo haya ya viwanda ili mambo yaende sambasamba na sera yetu ya Uchumi wa Buluu.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa niseme kwamba, kuna maeneo tengefu ambayo yamewekwa kwa ajili ya viwanda. Ukiangalia kuna maendeleo ya Dunga, Amani, Maruhubi na hata Fumba. Mimi niwaombe serikali na niseme kwamba haya maeneo kwa hapa Unguja nahisi ni mengi na ukizingatia maeneo ya viwanda yawe maeneo maalum ili zile athari ambazo zinatokana na viwanda hivi zisije zikasambaa kwenye maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, kuna mchangiaji hapa leo asubuhi amegusia namna ya kuweza kuondosha na kuharibu mazingira kutokana na hivi viwanda vyetu. Mfano, Juzi tulikizungumzia Kiwanda cha Makonyo kwamba kuna baadhi ya uharibifu ambao unatokea kutokana na viwanda hivyo. Kwa maana hiyo, ushauri wangu kwenye hii sekta naiomba wizara irudi na iangalie maeneo tengefu haya ya viwanda ili tuseme kwamba eneo hili ni kwa ajili ya viwanda pekee na eneo hili ni kwa ajili ya matumizi mengine. Ili kuondosha viwanda hivi ambavyo vipo kila sehemu, kila pahali unakuta kiwanda na hata uharibifu wa mazingira utachangia kwa asilimia kubwa sana.

Kwa hiyo, niwaombe wizara na serikali kwa ujumla na nadhani serikali ipo imetulia pale mbele, ione haja ya kurudi tena kuyaangalia maeneo haya kwa kunusuru wananchi wetu lakini kunusuru hali halisi ya mazingira ya tabianchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye jambo jengine kwenye kipa umbele namba kumi kwenye kifungu kidogo namba 5, kwenye vipaumbele hivi wamesema kwamba kuna kuandaa mpango wa kuwepo eneo maalum la mji wa kiserikali. Nadhani hii itaenda sambamba na ile hoja ya kuhusiana na maeneo ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika, tunapoelekea sasa hivi niipongeze sana serikali kwa kuliona jambo hili muhimu na lina afya na tija kwetu sisi. Kwa sababu nchi nyingi ukiziangalia zinazoendelea basi kuna maeneo maalum ambayo wameyatenga kwa sababu ya kiserikali na maeneo haya wenyewe wanayatamka kama ni *presidential area*. Kwa maana hiyo, kama kwetu sisi tumeamua na tumeweka mpango huo iwe kama ni mpango maalum kwa ajili ya maeneo ya serikali yetu basi niiombe serikali izingatie maeneo haya kuyapelekea miundombinu halisi ya kufikika lakini miundombinu halisi ama mazingira rafiki ya kuweza kuwaweka viongozi wetu wa serikali.

Mhe. naibu Spika, hapa ninataka kushauri kwamba maeneo haya au mji huu kiserikali ujumuishe majengo yote ya viongozi wakuu. Lakini ijumuishe maofisi ya serikali na hii itatusaidia kwamba kila pahali unapokwenda unakutana na ofisi ya serikali hii na nyengine unaikuta huku. Kwa maana tukiweka eneo maalum la kuona kwamba tukiwa tuna shida zote za kiofisi basi twende eneo fulani tukatatue changamoto zetu. Lakini tukisema tuna shida ya viongozi wetu wakuu tunajua tunaenda eneo fulani ya kuweza kukutana na viongozi wetu. Hii itatusaidia hata kuondosha foleni zilizokuwa hazihitajiki kwenye maeneo yetu hasa wakati wa ziara za Waheshimiwa Viongozi wetu wakuu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kugusia kipa umbele cha 16 ambacho kimegusia, kuendelea kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wake. Mimi hapa naomba niseme kwamba azma ya serikali yetu na Mapinduzi yetu Matukufu ya Zanzibar ni kuwaletea huduma wananchi wao na kwa bahati njema tuiipongeze sana serikali yetu kupitia Mamlaka ya Maji *ZAWA*, wanajitahidi kwa namna ambavyo Mungu kawajaalia na nguvu zao. Lakini hapa tuwaombe kila Mhe. Mwakilishi, akisimama hapa anagusia suala la maji na kwa bahati njema Mhe. Waziri wa Maji na Nishati, hajawahi kukosa swali la nyongeza hata siku moja. Kila anapojaribu kujibu maswali pale mbele basi wawakilishi wengi husimama kwa ajili ya kutetea tatizo hili. Kwa maana hiyo niiombe serikali kama Mwakilishi wa wananchi, tuone namna bora ya kuweza kutatua changamoto hii ili tupunguze hizi kelele za wananchi kila siku.

Mhe. Naibu Spika, leo hii nimesikia habari ambazo zilikuwa zinatolewa na Mamlaka ya Maji na Nishati, wanagusiua na wanahamasisha ulipaji wa maji tena maeneo ya Makunduchi. Niseme tu kwamba wananchi wetu sio kwamba hawataki kulipia huduma ya maji lakini upatikanaji wa huduma hii bado upo chini. Mimi nimefurahi kuona kwamba ajenda hii ipo kwenye vipaumbele vyetu. Kwa maana hiyo, serikali kama ipo vizuri na ipo macho kwenye eneo hili ijaribu kutafuta namna nyengine ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu ili huduma hii ipatikane vizuri.

Lakini kuna fedha ambazo zinaingizwa kila mwaka kwa ajili ya miradi ya maji, kuona changamoto hizi angalau zinapungua lakini bado kuna tatizo. Mhe. Waziri wa Maji na Nishati

yupo hapa aje kutupa *figure* ambayo inatuonesha kwamba tatizo hili litapungua kwa asilimia ngapi,na pia tumejiekeza kuliondosha kwa muda gani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo. Mimi naendelea kuipongeza Hotuba hii kwamba ipo vizuri, Mwelekeo wa hali ya Uchumi naamini utakwenda vizuri lakini pamoja na hayo twende sambamba na maisha halisi yetu ambayo tupo nayo.

Baada ya kusema hayo naipongeza sana wizara na naitakia utekelezaji mwema na mafanikio katika utendaji wake. Nakushukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, mchangiaji wetu anaefuata ni Mhe. Harusi Said Suleiman baadae ajitayarishe Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis.

**Mhe. Harusi Said Suleiman:** Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa maendeleo na Bajeti ya Mwaka 2020-2021-2022 mpaka 2024.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii niungane na wenzangu kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ufanisi wake mzuri wa kuweza kuiwasilisha hotuba hii kwa ujasiri.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii baada ya kuwasilishwa tuliifahamu na tuliielewa na ndio maana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anapata michango mingi. Napenda pia nichukue kumshukuru na kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na yeye kwa kuwasilisha taarifa ya kamati yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hotuba imeandaliwa vizuri, tukiangalia mwelekeo wa maendeleo, shabaha na malengo ya uchumi, vipa umbele na kadhalika kwa miaka yote hii ni mambo ambayo yanatekelezeka.

Hivyo, naiomba serikali iweke mikakati ya utekelezaji kwa watendaji wake vyenginevyo tunaweza tusifikie malengo tuliyoyakusudia kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo sababu ya ubinafsi, ufisadi wa rushwa na sababu ya kukosekana kwa uzalendo kwa wale watekelezaji wa miradi hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba nianze kuchangia kidogo na nianze na vipa umbele vilivyoainishwa katika hotuba hii na nianze na kipa umbele namba moja katika uk.21, kuimarisha miundombinu. Uimarishaji wa miundombinu ni jambo muhimu sana. Miundombimu ambayo imeaninishwa humu ni meiundombinu mbali mbali ikiwemo ujenzi wa barabara mbali mbali, viwanja vya ndege, ujenzi wa bandari na kadhalika.

Mhe. naibu Spika, naiomba sana serikali iachane na tabia ile ya kuamini sana vitengo vinavyohusika na maamuzi ya kuwapatia au kuwapitisha wakandarasi wa miradi, serikali kwa sasa ni lazima ijiridhishe kupitia wakandarasi hawa ambao watapitishwa na vitengo vinavyohusika.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tulipokuwa katika ziara tumejionea mambo mbali mbali ambayo unayaona wazi wazi kuwa wakandarasi waliopewa mradi huo hawana uwezo wa kutekeleza. Muda mrefu umeshapita, mradi ndio kwanza upo katika asilimia ndogo, muda uliobakia ni haba na hautoshi kumalizika kwa mradi huo na pesa za serikali zimeshakwenda, kwa kweli inasikitisha sana. Miradi imeanzia Unguja utekelezaji wake lakini itamalizia Pemba basi Unguja iko katika asilimia 75 lakini Pemba upo katika asilimia 0 na muda uliobakia ni mfupi wa miezi michache. *Imagine* wewe mwenyewe unapata shida hivi muda huu uliobakia wa miezi 15 kweli wataweza kumalizia hapa halafu wakaanze na miradi mengine Pemba. Ni dhahiri kwamba si rahisi bali pesa ya serikali inamung'unywa.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kusema kwamba barabara ya wete ni kongwe sana lakini pia ni barabara iliyo mbovu sana. Wananchi wanapita wanaitumia lakini ni barabara ambayo kwa kweli haina uwezo tena. Hivyo, inahitaji mkandarasi madhubuti, mkandarasi makini lakini pia inahitaji mkandarasi mwenye uwezo na vifaa vya kuweza kufanyia kazi. Hii si kwa barababara ya Wete-Chake tu ni barabara karibu zote za Pemba ambazo hazijapata ufadhili wa kutengenzwa.

Mhe. Naibu Spika, *geography* ya Pemba tunaifaham ni *geography* ya milima, mabonde pamoja na *cross* nyingi. Sasa tusipotumia ujasiri wa kuwapata wakandarasi ambao wana uwezo mzuri mkubwa na vifaa vya kutosha vya kisasa tutashtukia barabara zinajengwa tunakabidhiwa tunafurahi tunaimba nyimbo tunapokabidhiwa barabara hizo lakini matokeo yake baada ya miezi mitatu barabara zinaanza kutoa tena vumbi, mchanga, dongo na kupelekea usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo kwa upande wa barabara naomba niende katika kipa umbele chengine ambacho kipo katika ukarasa wa pili kufungu (e) kuimarisha sekta ya uchumi. Mhe. Naibu Spika, kuimarisha sekta ya uchumi kuchukua hatua maalumu za kusaidia zao la karafuu. Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu kwa kweli lilikwishapotea na wakulima walishakata tamaa muda mrefu wa kulishughulikia zao la karafuu na walifika kusema kwamba ni bora tuuze mabungo tutapata faida kulikoni kushughulikia karafuu, na hawakusema tu walikuwa wanatekeleza. Ilifikia hatua mikarafuu ilikuwa inachomwa moto lakini mikarafuu ilikuwa inatengenezwa mkaa, mikarafuu ilikuwa inafanywa kwamba ni miti ambayo ina nguzo au mbao nzuri za kutengenezea nyumba za wananchi kutokana na kulishusha thamani zao hilo.

Tumshukuru Mwenyezi Mungu katika awamu ya sita na saba Mhe. Rais Ali Mohammed Shein aliliona tatizo hili na akaongeza bei katika zao la karafuu, akatoa ahadi ya kuwaongeza tena na zao la karafuu likaendelea kuinuka na kurudi mikononi mwa serikali. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli katika kipindi kile tulipoteza pesa nyingi za serikali, maana hata kama mtu alitokea akasema yeye mimi ni jasiri nitachuma karafuu zangu siziwachi zikapotea basi alikuwa hauzi katika shirika la *ZSTC*. Matokeo yake alikua karafuu anaziuza Kenya, katika nchi jirani. Sasa hali ikawa ni ile ile serikali inakosa mapato kupitia zao la karafuu. Tuendelee kumshukuru Mhe. Dkt Ali Mohammed Shein kwa kurudisha zao la karafuu mikononi mwa wananchi lakini kulirudisha zao la karafuu mikononi kwa serikali kwa kuongeza bei ya uuzaji na ununuaji wa karafuu. Wananchi hususan wananchi wa Pemba wanaendelea kumshukuru Mhe. Dkt Ali Mohammed Shein kwa ujasiri huu mkubwa ambao aliuonesha.

Mhe. Naibu Spika, katika kuchukuwa hatua za kulisaidia zao la karafuu niombe serikali kuangalia uwezekano wa kuwapatia Bima za Afya wakulim awa zao la karafuu. Mhe. Naibu Spika, wakulima wa zao la karafuu ni wakulima ambao wanatatizo kubwa. Inapofika kipindi cha uchumaji wa karafuu Mhe. Naibu Spika, basi hali za roho zao huwa zimo kwenye mashaka, wanhamu waende wakachume karafuu kwa sababu ni zao ambalo linawapatia pesa tena haraka haraka huwa wameshaweka malengo kwamba mara hii nikichuma karafuu basi nahakikisha nanunua gari au mara hii nikichuma karafuu nahakikisha najenga nyumba yangu lakini huwa wanapambana na changamoto nyingi ikiwemo changamoto ya kupata ajali ya kuanguka mkarafuu.

Asilimia kubwa ya wachumaji karafuu ni vijana lakini wapo pia watu wazima ambao hawana uwezo tena lakini kwa sababu wanaitaka pesa wameshaweka malengo hawaangalii mkarafuu una urefu gani, una ukubwa gani yeye anachokiangalia juu ya mkarafuu ipo karafuu basi atapanda juu ya mkarafuu achume karafuu na matokeo yake wengine huwa wanakosa uwezo na Mwenyezi Mungu ameshaandikia kuanguka. Hupelekea vifo na wengine hupelekea kupata ulemavu wa maisha. Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali izidi kusimamia kuimarisha uchumaji wa karafuu kwa kuwapatia wakulima wa karafuu vifaa mbali mbali na hili ni jambo ambalo linawezekana kwa sababu tunawaona wafanyakazi wa Shirika la Umeme wanapanda kwenye nguzo za umeme kwa sababu ni nguzo ya hatari lakini kuna vifaa ambavyo vinamzuia yeye asiweze kuanguka kwa haraka. Kwa hivyo naiomba serikali iangalie uwezekano wa kupata vifaa vya kumsadia mchumaji wa karafuu akiwa juu ya mkarafuu kuweza kumdhibiti ili inapotokea upepo inapotokea kukosea kukanyaga katika tawi amablo alilolikusudia basi asiweze kuanguka kirahisi bali kuwe na kitu cha kumshikilia kuweza kuokoa maisha yake.

Mhe. Naibu Spika, niombe pia serikali katika zao hili la karafuu lisimamie uimarishaji wa ulinzi katika kudhibiti magendo ya karafuu. Ni dhahiri kwamba pamoja na kwamba ulinzi wetu ni mzuri ni madhubuti na mara nyingi tunasikia jinsi walivyokamata karafuu walivyokamata magendo ya mambo mengine lakini bado karafuu zinatoroshwa nje ya nchi, kwa sababu anaechuma karafuu ni binaadamu na binaadamu ana rai ana njia mbali mbali hata ukipita huku yeye anapita huku wanazichuma, wanaziuza nyengine wanazihifadhi ndani ya nyumba kwa muda inaweza kukaa karafuu hata kwa mwaka mmoja baadae ikatolewa ikapelekwa pwani na kusafirishwa. Sasa naiomba sana serikali iweze kudhibiti hali hii ili tusipoteze sana pesa zinazopatikana kupitia zao la karafuu. Mwisho kwa vile ushanihimiza naomba nizungumzie katika ukurasa 23 ujenzi wa nyumba za makaazi ya wananchi. Mhe. Naibu Spika, kujenga nyumba kwa ajili ya makaazi ya wananchi ni vyema lakini pia naomba serikali iangalie kuziangalia nyumba au miji tulionayo sasa iwe katika hali nzuri. Isiwe tunajenga nyumba mpya lakini hii mitaa yetu tunayoishi sasa haitazamiki.

Mgeni akija kwanza atafikia hata katika mitaa hii ya zamani ndio baadae atapelekewa katika miji mipya. Baadhi ya mitaa yetu sio mizuri inahitaji kuimarishwa na kuwekwa katika makaazi mazuri. Sio lazima zivunjwe nyumba zejengwe nyengine kama tulivyofanya Kwahani lakini tunaweza tukazuia ujenzi holela unaondelea. Zamani nyumba zilikuwa zimejengwa vizuri kiasi kwamba baskeli au gari inaweza kupita lakini sasa mtu akiongeza basi anavunjiwa.

Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Harusi Said. Mchangiaji anafuata ni Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis na baada ya hapo atafuata Mhe. Haji Omar Kheir.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya muelekeo wa hali ya uchumi mpango wa maendeleo na bajeti kwa mwaka 2021, 2022, 2023 na 2024. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenipa pumzi ya kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hotuba hii, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa utekelezaji wake wa ilani ndani ya siku 100 ambao umeleta matumaini makubwa kwetu sisi wazanzibari na namuomba Mwenyezi Mungu amuongezee nguvu ili yale yote ambayo aliyapanga yaweze kutimia.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Bajeti ambae ametoa ripoti yake hapa mbele ya Baraza lako ripoti ambayo imegusa kila vipengele vya uchumi na mpango wa maendeleo kwa kweli nampongeza sana na umahiri wake katika uwasilishaji. Lakini bila ya kumasahau Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa namna alivotuwasilishia taarifa hii kwa uweledi mkubwa na utulivu mkubwa tukaweza kufahamu hata michango naona jinsi ambavyo imeenda kwa kweli mpango huu ni mzuri.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba hii ukurasa wa 21 katika vipa umbele vya kitaifa kwa mwaka 2021 – 2022. Mhe. Naibu Spika, kipa umbele namba mbili kinasema kuimarisha sekta kuu za uchumi. Mhe. Naibu Spika, katika kumarisha sekta kuu za uchumi inazungumzia (a) kuimarisha uchumi wa buluu ikiwemo viwanda vidogo vidogo na vya kati vikiwemo vya usarifu wa mwani, chumvi na samaki kuendeleza shughuli za uvuvi wa bahari kuu na ujenzi wa mbwawa ya kufugia samaki, kuendelea na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Mhe. Naibu Spika, dhana ya uchumi wa buluu ni mpya, na kwa mujibu wa mpango wa serikali inahitaji wananchi wailelewe kwa vizuri na waifahamu. Kwa sababu zaidi imelenga kumuinua mwananchi mwenye kipato cha chini wakiwemo kundi la wanawake.

Kwa hiyo hili tufikie malengo ambayo serikali imepanga ni vizuri dhana hii ikatolewa elimu kwa wananchi hasa wa vijijini kwa sababu ni shuhghuli ambazo wanazifanya lakini hawaelewei kwa namna gani serikali imepanga kwa zile zile shughuli wanazozifanya waweze kuinua kipato chao. Kwa hiyo niiombe serikali katika hili ijitahidi kutoa elimu waende vijijini wakakutane na vikundi mbali mbali vya wavuvi, vya wanawake ambao wanajishuhulisha na ukulima wa mwani ili waieleze ile dhamira ya serikali kwa wananchi wetu hasa kupitia hizi shughuli ambazo wanazifanya kulekea uchumi wa buluu. Sasa hivi ukienda kijijini mtu anazungumzia uchumi wa buluu lakini ukimuuliza nini uchumi wa buluu hafahamu. Kwa hiyo niombe serikali ifanye hivyo ili wananchi waweze kutambua na serikali iweze kutimiza lengo lake.

Mhe. Naibu Spika, tunazungumzia uchumi lakini katika kuimarisha uchumi ni vyema pia tukaangalia maeneo mengine. Mimi Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo hua mara nyingi linanikereketa na niombe niishauri serikali yangu. Tuna vikosi vyetu viwili vya ulinzi, tunavyo vingi lakini navizungumzia viwili. Kikosi cha Jeshi la kujenga Uchumi na kikosi cha Chuo cha Mafunzo. Mhe. Naibu Spika, vikosi hivi ukiangalia JKU, JKU wanakusanya vijana wengi kwa

lengo la kuwajenga uzalendo, ukakamavu na masuala mengine. Lakini vijana wale wanapokwenda pale huwa mara nyingi dhana yao kwenda JKU unatafuta njia ya kupata ajira lakini mimi naamini wanafahamishwa jinsi ya kujiimarisha kiuchumi, kujijenga kizalendo na kiukakamavu. Niishauri serikali yangu katika hili ili tuimarishe uchumi uzuri zaidi kikosi cha JKU wawafundishe vijana pia katika suala zima la kilimo na ufugaji. Kwa sababu vijana wale watakapolima kilimo cha biashara wakaona ile faida ambayo inapatikana pale sifikirii atakapotoka pale ataanza kufikiria kuajiriwa katika jeshi, lakini wakati anasubiria ajiria basi ataweza kuanza na ule uchumi wa kutafuta kwa ajili ya kilimo. Atajikita katika kilimo kwa sababu faida ameshaijua.

Huku anasubiria ajira nyengine atakapopata ajira ataweza kwenda ajira lakini hakupata ajira kilimo na ufugaji vitaweza kumsaidia. Pia kikosi cha JKU wataweza kupunguza utegemezi wa bajeti ya serikali. Kwa sababu watapata chakula wao wenyewe cha kujilisha katika jeshi lao lakini pia wataweza kuhudumia mambo mengine madogo madogo na huku katika serikali kuu bajeti wataipunguzia mzigo. Katika Chuo cha Mafunzo vile vile wataweza kuzalisha, watahudumia wanafunzi waliomo ndani ya chuo.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mwantatu Mbarak naomba kwa sababu ya dharura maalumu ambayo nimeipokea kutoka kwa Mhe. Spika, kwamba tuakhirishe kikao na tayari mawaziri wameshatoka wameitwa kwenye Baraza la Mapinduzi lakini vile vile na kwa sababu ya kamati ya uongozi ya hapa kukutana inabidi sasa niakhirishe kikao Mhe. Mwantatu Mbarak utaendelea baadae kwa mujibu wa muongozo ambao tutapewa kwa hiyo naomba sasa nimwite waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kutengua kanuni ili tughairishe kikao hiki. Mhe. Waziri karibu.

## KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Naibu Spika, kwa vile mawaziri wengi wamepata dharura na kutoka naomba kutoa hoja kwamba Baraza liakhirishwe hadi leo jioni na sababu kubwa ni kwamba hoja inayowasilishwa hapa ni muelekeo wa mpango wa maendeleo na bajeti ambao unawagusa mawaziri wote kwa hiyo naomba kutoa hoja tuakhirishe hadi jioni leo hii.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Waziri, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kama alivyoelezea Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwamba tunaakhirisha na kwa makubaliano yenu wajumbe tunaakhirisha kikao hiki hadi leo jioni saa 11:00 hii leo ahsanteni.

*(Saa 6:30 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba kuarifu kuwa katika kutimiza matakwa ya sheria kwa mujibu wa sheria ya kuwaenzi viongozi wa kitaifa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameutangazia umma kuwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad amefariki dunia asubuhi ya leo. Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wajumbe na Baraza la Wawakilishi wa ujumla tunatoa pole kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, familia ya marehemu, chama chake cha ACT Wazalendo, Wazanzibari wote na Watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wetu huyo.

Tunamuombea dua Mwenyezi Mungu amsamehe dhambi zake na amjaalie pepo. Kufuatia msiba huo wa kitaifa uliotupata sote isingekuwa vyema kuendelea na shughuli zetu za Baraza na kwa hivyo tunaliakhirisha Baraza ili Waheshimiwa Wajumbe tuweze kushiriki katika msiba ikiwa ni pamoja na kumsindikiza kiongozi wetu huyu katika maziko yatakayofanyika kesho. Kwa msingi huo Waheshimiwa Wajumbe napenda kuakhirisha shughuli zetu hadi siku ya Jumatatu tarehe 22 Februari, 2021 saa tatu kamili za asubuhi. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

*(Saa 11:05 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka<br>tarehe 22/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*